**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# MAFANIKIO YA MIAKA 50

## TUMETHUBUTU, TUMEWEZA ,TUNAZIDI KUSONGA MBELE



**October 2011**

*TUMETHUBUTU, TUMEWEZA, TUNAZIDI KUSONGA MBELE*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# MAFANIKIO YA MIAKA 50 - VIWANDA

## TUMETHUBUTU, TUMEWEZA, TUNAZIDI KUSONGA MBELE



**October 2011**

6:2:5:3 Maeneo kwa ajili ya Vituo vya Pamoja vya Mipakani 47
6.2. 6.1 Ushindani huru na wa haki 48
6.2.6.2 Kuongezeka kwa ubora wa bidhaa 48
6.2.6.3 Kuboresha biashara ya ndani. 49
6.2.7 Utoaji wa elimu na mafunzo ya biashara (CBE, SIDO, TANTRADE) 49
6.3 Sekta ya Masoko 50
6.3.1 Kuboreshwa kwa masoko 50
6.3.2 Kuboresha utoaji wa lesseni 51
6.3.3 Utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara BARA 51
6.3.4 Kukamilika Uandaaji wa Sera ya Leseni za udhibiti, Sera ya Masoko na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Masoko. 51
6.3. 5.0 Kuboresha mfumo wa masoko ( mfumo wa stakabadhi ghalani) 52
6.3.5.1 Uhakika wa bei ya bidhaa 53
6.3.5.2 Mkulima kuunganishwa na asasi za fedha 54
6.3.5.3 Mikopo iliyotolewa kwenye vikundi na Asasi za fedha 2009/10 55
6.3.6.0 Kuboresha mfumo wa ununuzi wa mazao. 55
6.3.8.0 Fursa za masoko (maonyesho ya bidhaa ndani na nje, TANTRADE, SIDO, Vituo vya Biashara – Dubai, London) 57
6.3.9.0 Uanzishaji na uimarishaji wa Haki miliki (COSOTA) 58
7.0 Changamoto 58
7.1 Changamoto zilizojitokeza katika ngazi ya Wizara 58
7.2 Changamoto katika ngazi za Taasisi 59
7.3 Matararajio ya Wizara na Taasisi katika miaka hamsini (50). 60

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **BRELA** | Wakala wa Usajili na Leseni |
| **CAMARTEC** | Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini |
| **CBE** | Chuo cha Elimu ya Biashara |
| **COSOTA** | Chama cha Hakimiliki Tanzania |
| **DTC** | Kituo cha Biashara Dubai |
| **EPZA** | Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa Mauzo Nje ya Nchi |
| **FCC** | Tume ya ushindani |
| **FCT** | Baraza la Ushindani Tanzania |
| **NDC** | Shirika la Maendeleo la Taifa |
| **SIDO** | Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo |
| **Tan Trade** | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania |
| **TBS** | Shirika la Viwango la Tanzania |
| **TCCIA** | Chama cha Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo |
| **TEMDO** | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania |
| **TIC** | Kituo cha Uwekezaji |
| **TIRDO** | Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania |
| **TLWB** | Bodi ya Leseni za Maghala |
| **TRA** | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **TPSF** | Taasisi ya Kuendeleza Sekta Binafsi Tanzania |
| **WMA** | Wakala wa Mizani na Vipimo |

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Historia fupi ya Wizara

Tangu mwaka 1961 majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara yamekuwa yakibadilika kutokana na mabadiliko ya kimuundo kwa vipindi saba tofauti. Kati ya mwaka 1961-1965, Wizara ilisimamia sekta za Biashara, Viwanda na Madini na ilikuwa ikiitwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Madini. Kati ya mwaka 1965 hadi 1967, Sekta za viwanda na biashara zilitenganishwa na kuwepo kwa Wizara ya Viwanda na Nishati iliyokuwa ikisimamia sekta za viwanda, nishati na madini na Wizara ya Biashara na Ushirika iliyosimamia sekta za Biashara na Ushirika.

Kati ya mwaka 1967-1975 sekta za Biashara na Viwanda ziliunganishwa tena na kuunda Wizara ya Biashara na Viwanda. Katika kipindi hiki majukumu ya Wizara yalikuwa kusimamia sekta za viwanda, Biashara, madini na nishati.

Kati ya mwaka 1972 na 1975, sekta ya madini iliachwa katika Wizara ya Viwanda na Biashara na ile ya Nishati ilihamishiwa Wizara nyingine. Baadaye mabadiliko yalifanyika kufutia mahitaji ya uemdelezaji wa viwanda vya msingi (Basic Industry Strategy) mwaka 1975 na kubakia Wizara ya Viwanda hadi mwaka 1984. Kuanzia mwaka 1984 hadi mwezi Desemba mwaka 2005 Wizara iliitwa Wizara ya Viwanda na Biashara ikiwa na jukumu la kusimamia sekta za viwanda na Biashara. Mwaka 2006 kupitia *Presidential Circular No.2* ya mwaka 2006 sekta ya masoko ilihamishwa kutoka Wizara ya Ushirika na Masoko na kuunganishwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Jina la Wizara lilibadilika na kuwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kupitia gazeti la Serikali No. 420 la mwaka 2010 jina la Wizara lilirejea tena kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara lakini ikibaki na majukumu yale yale ya kusimamia sekta za Viwanda, Biashara na Masoko.

Wizara ya Viwanda na Biashara ina Idara sita na vitengo sita. Idara hizo ni Idara ya Sera na Mipango, Idara ya Mtengamano wa Biashara ya Kimataifa, Idara ya Maendeleo ya Viwanda, Idara ya Maendeleo ya Masoko, Idara ya Viwanda Vidogo na Biashara ndogo na Idara ya Utawala na Maendeleo ya Utumishi. Vitengo ni Kitengo cha Uhasibu, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha Elimu, Habari na Mawasiliano, Kitengo cha MIS, Kitengo cha Ugavi na Kitengo cha Sheria.

Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inashirikiana na taasisi zilizo chini yake ambazo kwa ujumla wake ziko taasisi 17. Taasisi hizo zinajumuisha Mashirika matano (5), Vituo vitatu (3), wakala mbili (2), Mamlaka mbili (2), Chuo kimoja (1), Kamisheni moja (1), Tume moja (1), Bodi moja (1) na Chama kimoja (1).

## 1.2 Historia fupi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara

**Mashirika**: Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii ni matano. Mashirika hayo ni Shirika la Maendeleo la Taifa *(National Development Corporation - NDC)* ilianzishwa kama *Tanganyika Development Corporation (TDC)* tarehe 01 Januari 1962, baada ya Uhuru ili kuchochea maendeleo ya viwanda. Baada ya Muungano, chini ya Sheria ya Bunge ya tarehe 01 Januari 1965 NDC ilipewa majukumu mapya ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika sekta muhimu kwa maslahi ya Taifa ikiunganishwa na kampuni ya kilimo *(Tanganyika Agricultural Corp)*. NDC ilikuwa chini ya Wizara ya Uchumi na Mipango, Meneja Mkuu akiwa ni Mfaransa Bw. J. Faudon na Bodi iliundwa na Mawaziri chini ya uenyekiti wa Waziri P. Bomani ili kulipa nguvu stahiki shirika la NDC.

Novemba 1966 Meneja Mkuu Mpya Bw. George Kahama aliteuliwa na Shirika la Mwananchi Development Corporation likaunganishwa na NDC wakati huo ofisi za Shirika zikiwa Jengo la Ushirika kabla ya kuhamia Jengo la Maendeleo 1968. Sheria ya NDC ya 1965 ilirekebishwa mwaka 1969 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma na kuipa NDC mtaji na uwezo wa kisheria wa kujiendesha kibiashara.

Kati ya 1965 na 1996 NDC ilipitia vipindi mbalimbali vya mabadiliko ya kisheria, kisera na mageuzi ya kiuchumi ya Mashirika ya Umma ya 1992 iliyorekebishwa 1993 wakati makampuni tanzu yaliwekwa chini ya "***The Presidential Parastatal Sector Reform Commission*** (PPSRC).

**Kati ya 1965 na 1969,** NDC ilichangia sana kujenga "**viwanda na makampuni ya kibiashara**" na mengine yaliyopevuka na kuondolewa NDC ili yajitegemee mwaka 1969 kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania Tourist Corp (TTC) | Tanganyika Packers Ltd(TPL) | National Textile Co (NTC) |
| National Agricultural & Food Corporation (NAFCO) | National Estates and Designing Corp (NEDCO) | Cashewnuts Authority of Tanzania (CAT) |
| Small Industries Development Corporation (SIDO) | Mwananchi Engineering & Contracting Co Ltd (MECCO) | State Mining Corporation (STAMICO) |
| Tanzania Wood Industry Corporation (TWICO) | Tanzania Tobbaco Processing Company (TTPC) | Tanzania Standard Newspaper Ltd (TSN) |

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania Elimu Supplies (TES) | Tanzania Sisal Corp (TSC) | Tanzania Dairies Ltd (TDL) |
| Tanzania Pyrethrum Board | | |

**Kati ya 1970 na 1980,** NDC ilikuwa kichocheo kikubwa katika usimamizi na uanzishaji wa makampuni mapya na kuanzisha viwanda kama kituo cha kukuzia na kulelea wataalam wazalendo. Wataalam walishika menejimenti za mashirika mengi ya umma na binafsi nchini, hususan, ya sekta za uzalishaji na biashara. Itakumbukwa kuwa changamoto kubwa mara tu baada ya uhuru na hatimaye katika utekelezaji wa siasa ya "**Ujamaa na Kujitegemea**" ilikuwa ni upatikanaji wa wataalam wazalendo kusimamia uendeshaji wa uchumi wa nchi na NDC ilitimiza jukumu hili kwa umakini sana.

Pamoja na mtikisiko wa uchumi wa miaka ya 1973 hadi 1975 ulioitikisa nchi, NDC ilishiriki kikamilifu kukuza uchumi hususan kati ya 1976 na 1977 na kipindi hiki kilikuwa sio kizuri sana baada ya kuyaondoa makampuni yake tegemezi kuondolewa mwaka 1979 na 1980. Makampuni haya ni haya yafuatayo:-

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania Karatasi Assiciated Industries (TKAI) | Tazania Leather Associated Industries (TLAI) | Tanzania Breweries Limited (TBL) |
| Tanzania Coffee Authority (TCA) | Tanzania Cigarette Company (TTC) | |

**Kati ya 1980 hadi 1996,** NDC pamoja na kusimamia viwanda vya kiuchumi, kuelimisha wazalendo nchi mbali mbali duniani ilijikuta ikilazimika na marekebisho ya mashirika ya 1993, kupitia PSRC na kuondoa hisa ilizokuwa inazimiliki na kuzihamisha kwenda kwa Msajili wa Hazina (Treasury Registrar) na kuiachia NDC madeni (contingency liabilities).

Makampuni yaliyobinafsishwa kufikia mwaka 1996 na kuondolewa NDC ni:-

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania Crown Cork Co. Ltd | National Engineering Co. | National Textile Co (NTC) |
| National Steel Corporation | Tanzania Motor mart Co. Ltd | Tanzania Metal Box Ltd |
| Aluminium Africa Co Ltd | Tanzania Light Source Indust | Ubungo Farm Implement |

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania Oxygen Ltd | National Bicycle Co. Ltd | Zana Za Kilimo Mbeya |
| Mang'ula Mechanical & Machine Tools Co. Ltd | Tanga Steel Rolling Mills | TANELEC |
| Tanzania Cables Ltd | | |

Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*Small Industries Development Organization - SIDO)* lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge ya mwaka 1973 kwa ajili ya kupanga, kuratibu, kuendeleza na kutoa huduma mbalimbali katika sekta ya viwanda, biashara ndogo na Biashara za Kati.

Shirika lina ofisi katika mikoa yote ya Tanzania bara lengo likiwa kuendeleza wajasiriamali wadogo kwa kuanzisha na kusaidia maendeleo ya tasnia ndogo na za kati za viwanda na biashara. Kimpaumbele kinatolewa katika sekta ya uzalishaji katika kuongeza kipato.

Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*Tanzania Industrial Research Development Organizationa - TIRDO)*- Hili ni Shirika la Umma lililoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 5 ya Mwaka 1979 na kuanza shughuli zake Mwezi Aprili, 1979. Kimsingi Shirika hili linashughulika na utafiti wa teknolojia za Viwandani na kutoa ushauri wa masuala ya kiteknolojia katika Sekta ya Viwanda.

Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo *(Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization – TEMDO )*- Shirika hili limeanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya Mwaka 1980 likishughulikia masuala ya uhandisi ns usanifu mitambo katika Sekta ya Viwanda.

Shirika la Viwango Tanzania (*Tanzania Bureau of Standards - TBS*) limeundwa chini ya Sheris ya Bunge Na. 3 ya Mwaka 1977 na baadaye kuanzishwa upya chini ya Sheria Na. 2 ya Bunge ya Mwaka 2009.

**Vituo**: Wizara ya Viwanda na Biashara ina vituo vitatu vikiwemo Kituo cha Zana za Kilimo na Utafiti Vijijini *(Centre for Agricultural Mechanisation of Rural Technology - CAMARTEC)* kimeanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 19 ya Mwaka 1981 na kuanza kufanya kazi zake Julai 1982 kikishughulika na ubunifu, usanifu, uhamasishaji na usambazaji wa teknolojia na zana za kilimo Vijijini.

Kituo cha Biashara cha London (*Tanzani Trade Centre - London*) kilianzishwa mwaka 1989 na kinaendesha shughuli zake katika ofisi za Ubalozi wa Ta nzania London nchini Uingereza.

Madhumuni ya Kituo hiki ni kukuza mahusiano ya kiuchumi kati ya Tanzania na Uingereza na pia nchi za jirani za Ulaya na hata nje ya Ulaya. Pamoja na jukumu hili kituo pia kina jukumu la kuvutia wawekezaji wa kigeni, utalii, ukuzaji wa Diplomasia ya Uchumi na kutoa taarifa na huduma za kibiashara.

Kituo cha Biashara Cha Dubai (*Tanzania Trade Centre – Dubai)* kilifunguliwa mwaka 2007 kwa lengo la kukuza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la nchi za Mashariki ya kati. Aidha Kituo hiki kinajukumu la la kuvutia wawekezaji kuwekeza nchini Tanzania pamoja na kuvutia Watalii kuja nchini. Ofisi za Kituo hiki zipo katka Ubalozi mdogo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliopo Dubai.

**Chuo:** Wizara ina chuo kimoja kiitwacho Chuo cha Elimu ya Biashara (*College of Business Education*) kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 31 ya mwaka 1965 kikiwa na Kampasi moja ya Dar es Salaam. Mwaka 1983 Chuo kilifungua kampasi ya Dodoma na Mwaka 2007 kikaongeza kampasi nyingine ya Mwanza.

**Mamlaka:** Wizara ina mamlaka mbili ambazo ni Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuuza Nje (*Export Procesing Zones Authority –EPZA)* ambayo ilianzishwa kama programu mwaka 2002 kupitia Sheria ya Bunge Na. 11. Madhumuni ya programu hii ilikuwa ni kuvutia wawekezaji kwenye Viwanda hasa vinavyouza nje ya nchi., kuongeza ajira, kuvutia matumizi ya teknolojia mpya na zaidi kuongeza thamani ya mazao na rasilimali zingine lengo likiwa kuondoikana na utegemezi wa bidhaa ghafi kwa mauzo ya nje.

Mwaka 2006 Serikali ilianzisha mfumo wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi kupitia Sheria ya Bunge. Lengo la mfumo huu ni kuweka vivutio kwa uwekezaji unaolenga Viwanda vinavyouza katika soko la ndani na uwekezaji katika kwenye sekta zingine kama utalii, huduma, kilimo n.k.

Mwaka 2011 mwezi Aprili Serikali imeunganisha mifumo yote hii miwili EPZ na SEZ kuwa chini ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuu Njee (EPZA) ili kupunguza gharama za uendeshaji na kukinzana katika utekelezaji wa adhma hii ya kujenga uchumi wenye nguvu.

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(The Tanzania Trade Development Authority – TANTRADE)* imeanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mwaka Na. 4 ya 2009 ikifuta Sheria ya Bunge Na.15 ya mwaka 1973 iliyoanzisha Bodi ya biashara ya Ndani (BIT) na Sheria Na 5 ya Mwaka 1978 iliyoanzisha Halmashauri ya Biashara ya Nje (BET). Mamlaka hii imeanzishwa ili kufanikisha utekelezaji wa Sera za Kisekta zinazosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Lengo kuu ikiwa kusimamia biashara ya ndani na kuhamasisha biashara ya nje

kupiti njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na maonyesho ya kibiashara ndani na nje ya nchi.

**Wakala**: Wizara ina wakala mbazo ni Wakala wa Mizani na Vipimo (*Weights and Measures Agency -WMA)* ilianzishwa kwa mujibu Sheria ya Wakala wa serikali Na. 30 ya mwaka 1997 iliyounda *Weights and Measure Bureau* iliyobadilishwa kuwa Wakala wa Vipimo kuanzia tarehe 13 Mei, 2002 kwa Tangazo la Serikali *(Order No. 194)* la tarehe 17 Mei, 2002. Wakala huu unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura 340 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002 na Sheria ya Wakala wa Serikali ya tarehe 17 Mei, 2002. Wakala huu unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura 340 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002 na Sheria ya Wakala za Serikali Sura Na. 245 kama ilivyorekebishwa mwaka 2009.

Awali, matumizi ya vipimo yalianza kabla ya uhuru kwa kutumia Metric system yaliyoanzishwa na Wajerumani wakati wa utawala wao kabla ya vita kuu ya dunia mwaka 1914-1918. Waingereza walipokuja nao waliingia na mfumo wa matumizi ya vipimo vya impreriao (*Imperical system of Measurements*) uliotumika sambamba na vipimo vya metriki.

Mwaka wa 1960 sheria hiyo ya vipimo ilifutwa na kuanza kutumika sheria mpya, *Weights and Measurements Ordinance, Chapter 426* ya mwaka 1960. Sheria hii iliiweka Idara ya Vipimo chini ya Wizara iliyokuwa ikihusika na masuala ya biashara ambayo ilikuwa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mwaka 1964, Idara ya Vipimo ilikuwa chini ya Wizara ya Biashara na Ushirika hadi mwaka 1967 iliporejeshwa katika Wizara ya Viwanda na Biashara ikioongozwa na Kamishna wa Vipimo. Mwaka 1968, Tanzania na nchi zingine za Afrika Mashariki (Kenya na Uganda) zilianza kutumia mfumo mmoja wa vipimo wa metriki. Mwaka 1969, Tanzania ilifungua ofisi za vipimo katika kanda tatu (Mwanza, Tanga na Mbeya). Ilipofika mwaka 1977/78 ofisi za vipimo zilienezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Sheria ya Weights and Measures Ordinance, Chapter 426 ya mwaka 1960 ilifutwa na sheria mpya, *Weights and Measures Act No. 20* ya mwaka 1982. Kuanzia 1984, *Weights and Measures Bureau* ilikuwa kitengo chini ya kurugenzi ya Biashara katika Wizara ya Viwanda na Biashara hadi ilipobadilishwa na kuwa Wakala wa Vipimo kuanzia mwaka 2002. Kwa kipindi chote hicho Wakala umekuwa ukitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Na. 20 iliyopitishwa na Bunge mwaka 1982 na kuanza kutumika rasmi tarehe 15 Mei, 1983 kwa Tangazo la Serikali Na. 59 la mwaka 1983.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni za Viwanda *(Business Registration and Licensing Agency - BRELA)* iliyoundwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997

na kuzinduliwa rasmi tarehe 3 Desemba, 1999. Wakala huu una dhamana ya kuwezesha na kudhibiti masuala ya usajili wa biashara.

**Kamisheni:** Wizara ina kamisheni moja tu ambayo ni Kamisheni ya Maadili ya Biashara *(Fair Competition Commission - FCC)* ambayo chimbuko lake ni kufutwa kwa Sheria ya udhibiti bei ya mwaka 1973 *(Price Control Act. 1973)*. Sheria hii ilifutwa Novemba, 1993 kutokana na mjadala wa Bunge uliooneshа haja ya kuwepo sheria na taratibu mbadala za kusimamia uchumi wa soko nchini. Hatua hii ilisabaisha kutungwa kwa Sheria ya Ushindani ya mwaka 1994.

Sheria hiyo ilibeba majukumu mengi hatimaye kusababisha kufutwa na Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 iliyotungwa pamoja na sheria zingiune nne zinzzo husu udhibiti wa makampuni ya biashara yenye ukiritimba asilia.

Tume ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake kama chombo chenye mamlaka kamili ya kusimamia sheria ya Ushindani na Sheria ya Alama za Bidhaa, inayotumika kudhibiti biashara ya bidhaa bandia ya Mwezi Mei, 2007. Katika kutekeleza wajibu wake kama mahakama maalum inayosikiliza mashauri ya ukiukwaji wa misingi ya ushindani kwa Mujibu wa Sheria ya Ushindani, Tume imesikiliza mashauri kadhaa yanayohusiana na sekta za Viwanda vya Bia, Tumbaku na Matangazo ya Barabarani.

**Baraza: Wizara** ina Baraza la Ushindani *(Fair Competition Tribunal - FCT)*. Baraza hili ni Chombo huru kinachojitegemea, kilichoundwa kwa mujibu kifungu cha 83 ya Sheria ya Ushindani Namba 8 ya mwaka 2003 kwa madhumuni ya kusikiliza rufaa ya mashauri ya kibiashara yanayofikishwa kwake baada ya maamuzi ya Tume ya Ushindani.

**Bodi:** Bodi ya Leseni ya Maghala *(Tanzania Warehouse Licensing Board - TWLB)* inasimamia mfumo wa Stakabadhi za Maghala ulioanzishwa kisheria kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 2005 na kutekelezwa kwa kanuni za mfumo za mwaka 2006. Mfumo huu sasa unatumika katika maeneo mbali mbali nchini kwa mazao ya Korosho, Kahawa, pamba, mpunga/mchele na mahindi.

Wakulima wa zao la kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma na Kigoma wametekeleza mfumo huu msimu wa 2002/2003. Maghala ya TCCCO, MBICCO, MBOCCO na Kanyovu Joint Venture- Kigoma yanatumika katika mfumo huu kuanzia msimu wa 2008/09.

Vyama vya Ushirika vya Msingi mkoani Shinyanga vimeanza kutumia mfumo huu kuanzia msimu wa mwaka 2007/08 kuhifadhi na kuchambua pamba katika jineri ya Uzogore chini ya mwendesha ghala-SIBUKA FM LTD.

Wakulima wa Korosho katika mkoawa Mtwara wameanza kutumia mfumo huu msimu wa mwaka 2007/2008 ambapo jumla ya vyama vya Msingi 164 viliwezeshwa kutumia mfumo huu. Aidha katika msimu wa mwaka 2008/2009 mfumo uliendelea kutekelezwa katika mkoa wa Mtwara na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Lindi na Pwani.

**Chama:** Chama cha Hakimiliki Tanzania (*Copyright Society of Tanzania COSOTA)* ni asasi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 64(1) Sheria mama ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999, Sura ya 218 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwa 2002. Kwa mujibu wa kifungu cha 47 cha sheria hii COSOTA ina jukumu la kulinda, kusimamia, kuikuza na kutetea maslahi ya watunzi.

## 2.0 MUUNDO WA WIZARA KUANZIA 1961

Muundo wa Wizara umekuwa ukibadilika kwa vipindi na nyakati tofauti kutokana na mabadiliko ya uongozi wa juu wa Serikali ambao hutumia mamlaka ya kikatiba kwa Rais, kupanga Wizara na Watendaji wa kumsaidia kutekeleza ilani ya uchaguzi ya chama chake ambacho kupitia uchaguzi wa kidemokrasia hupewa ridhaa na wananchi kwa upigiwa kura. Wizara imebadilika kwa kusimamia sekta mbalimbali na tofouti kama Jedwali hapa chini linavyoonyesha:

| JINA LA WIZARA | MWAKA |
|---|---|
| Wizara ya Biashara na Viwanda | 1962 -1964 |
| Wizara ya Biashara na Ushirika | 1964-1966 |
| Wizara ya Viwanda, Madini na Umeme | 1964-1965 |
| Wizara ya Viwanda, Madini na Nishati | 1965 -1966 |
| Wizara ya Viwanda, Madini na Umeme | 1966-1967 |
| Wizara ya Biashara na Viwanda | 1967-1976 |
| Wizara ya Viwanda | 1976-1986 |
| Wizara ya Biashara | 1976-1986 |
| Wizara ya Viwanda na Biashara | 1986-2006 |
| Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko | 2006-2007 |
| Wizara ya Viwanda na Biashara | 2010- sasa |

## 3.0 MAJUKUMU NA MALENGO YA WIZARA NA TAASISI

### 3.1 Majukumu ya Wizara

Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni yafuatayo:-

- Kuanzisha viwanda mama, kwa kutafuta wabia wa kuwekeza katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma, mradi wa chuma wa Liganga na tafiti za mirad mingine iliyo katika Kanda za Maendeleo;
- Kuimarisha usindikaji na kuhamasisha uanzishaji wa Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZ);
- Kufanya utafiti wa Maendeleo ya Viwanda;
- Kuendaa na Kutekeleza Mikakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta za kipaumbele kama vile ngozi, nguo, chuma, chakula, mbolea na vifaa vya ujenzi
- Kuandaa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya maendeleo ya viwanda;
- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Maendeleo Endelevu ya Viwanda na Maendeleo ya Viwanda Masoko ya mazao na bidhaa za kilimo, Maendeleo ya Biashara, Vidogo na Biashara ndogo;
- Kuimarisha Taasisi za utafiti, mafunzo na maendeleo;
- Kuendelea kuwezesha ubunifu na uenezaji wa teknolojia zinazofaa vijijini ili kurahisisha kazi ya uanzishaji wa viwanda vidogo, hususan vya usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao na bidhaa;
- Kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni mikakati ya kuendeleza sekta za viwanda, biashara na masoko kwa lengo la kukuza mchango wa sekta hizo katika maendeleo ya uchumi wa Taifa;
- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Mauzo nje;
- Kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa masoko ya kimataifa ya mazao ya kilimo na bidhaa;
- Kuendeleza na kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa

taarifa za viwanda, biashara na masoko;

- Kuimarisha uwezo wa Halmashauri na Manispaa wa kukusanya, kuhifadhi, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko;
- Kuwaelimisha wadau kuhusu maendeleo na fursa za masoko zilizopo ndani na nje ya nchi;
- Kufanya tathimini ya uboreshaji wa miundombinu ya masoko;
- Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo na utoaji wa huduma zinazolenga katika kuchochea kuanzishwa na kuimarishwa kwa sekta husika katika nyanja za ufundi, mafunzo na ushauri;
- Kuendeleza jitihada za kukuza soko la ndani kwa kukuza matumizi ya mazao na bidhaa, mbalimbali zinazozalishwa nchini;
- Kuendeleza utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao ya Maghala;
- Kuongeza ubora wa bidhaa, kupanua wigo wa masoko, kuhamasisha upatikanaji wa mitaji na kuimarisha usambazaji wa teknolojia zinazofaa kwa lengo la kuongeza tija; na
- Kuanzisha vituo vya biashara katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na kuongeza nafasi za ajira na kipato hususan kwa wanawake na vijana.
- Kushiriki majadiliano ya nchi na nchi kikanda na kimataifa katika juhudi za kutafuta fursa za masoko ya fedha zetu

Ili kutekeleza majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ufanisi, inafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kutekeleza Sera ya Viwanda Endelevu – *(Sustainable Industrial Development Programme - SIDP (1996-2020);* Sera ya Taifa ya Biashara, Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara ndogo na Sera ya masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Policy);*
(b) Kuandaa na kusimamia programu za kuendeleza sekta binafsi ili iweze kutoa mchango wake katika maendeleo ya uchumi wa Taifa;
(c) Kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta za viwanda, biashara na Masoko;
(d) Kusimamia utekelezaji wa Sheria zinazotawala viwanda, biashara na masoko;
(e) Kushirikiana kikamilifu katika majadiliano ya ushirikiano kwa lengo la kuhakikisha kuwa Tanzania inafaidika na ushirikiano na mikataba yote ya kibiashara;

(f) Kuimarisha taasisi za utafiti wa maendeleo ya teknolojia za viwanda ambazo ni rahisi, za kisasa, na zinazoendana na hali ya nchi kimalighafi;

(g) Kuweka taratibu, kukuza na kuimarisha ulinzi na haki za uvumbuzi na ubunifu (*intellectual property rights);*

(h) Kusimamia taratibu na sheria za biashara ikiwa ni pamoja na maadili ya ushindani katika uchumi ili kuliwezesha Taifa kuhimili changamoto ya biashara za kimataifa hususan chini ya utaratibu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) na kuimarisha ushirikiano kati ya nchi na nchi *(Bilateral)* wa kikanda na kimataifa.

(i) Kujenga sekta binafsi yenye nguvu itakayoshiriki katika uzalishaji/usindikaji na biashara ya mazao na bidhaa za kilimo na pembejeo.

(j) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu, masoko na biashara ya bidhaa za kilimo ikiwemo usindikaji wa mazao na ujenzi wa maghala.

(k) Kupitia na kurekebisha na kuhuisha sheria, kanuni na taratibu zinazotawala Sera mbalimbali zinazosimamia maendeleo ya sekta ya masoko. Kanuni ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala iliandaliwa na kuridhiwa. Mfumo huu umeendelezwa na kufanyiwa majaribio katika mazao mbalimbali kama vile mpunga, na mahindi. Aidha, mchakato wa kutumia mfumo huu kwenye zao la korosho umeanza.

## 4.0 Uongozi na utawala kuanzia 1961.

| JINA LA WAZIRI | JINA LA WIZARA | MWAKA |
|---|---|---|
| Bw. C.G.Kahama (Bukoba) | Biashara na Viwanda | 1962 -1964 |
| Bw. J.S.Kasambala (Rungwe) | Waziri wa Biashara na Ushirika | 1964-1965 |
| Bw. A.K.Hanga (Unguja) | Waziri wa Viwanda, Madini na Umeme | 1964-1965 |
| Bw. J.S.Kasambala (Rungwe) | Viwanda, Madini na Nishati | 1965 -1966 |
| Bw. A.M.Babu (Zanzibar) | Biashara na Ushirika | 1965-1966 |
| Bw. A.Z.Nsilo Swai (Arusha Urban) | Viwanda, Madini na Umeme | 1966-1967 |
| Bw. A.M. Maalim (Kateuliwa Zanzibar) | Waziri wa Biashara na Viwanda | 1967-1971 |
| Bw. P.Bomani (Nyanza) | Waziri wa Biashara na Viwanda | 1971-1974 |

| | | |
|---|---|---|
| Bw. A.H.Jamal (Morogoro) | Waziri wa Biashara na Viwanda | 1974-1976 |
| Bw. C.D. Msuya-(Kateuliwa) | WaziriWaziri wa Viwanda | 1976-1982 |
| Bw. A. Rulegura-(Sengerema) | Biashara | 1976-1982 |
| Luteni Kanali A.S.Mchumo (Temeke) | Biashara | 1982-1983 |
| Bw. Mustapha Nyang'anyi (Kondoa) | Biashara | 1983-1986 |
| Bw. Basil P.Mramba (Rombo) | Viwanda na Biashara | 1986-1989 |
| Mhe. J.C. Rwegasira – Mbunge wa Taifa | Viwanda na Biashara | 1989-1990 |
| Mhe. Cleopa D. Msuya (Mwanga) | Viwanda na Biashara | 1990-1995 |
| Mhe.Dr.William F.Shija (Sengerema) | Viwanda na Biashara | 1995-2001 |
| Mhe. Dkt. Abdallah Kigoda (Handeni) | Viwanda na Biashara | 1996-1997 |
| Mhe. Kingunge Ngombaremwiru | Viwanda na Biashara | 1998-1999 |
| Mhe. Iddi M. Simba (Ilala) | Viwanda na Biashara | 2001-2002 |
| Mhe. Dr. Juma Alifa Ngasongwa (Ulanga ) | Viwanda na Biashara | 2002-2005 |
| Mhe. Nazir M. Karamagi (Bukoba Vijijini) | Viwanda, Biashara na Masoko | 2006-2007 |
| Mhe. Basil P.Mramba (Rombo) | Viwanda,Biashara na Masoko | 2007-2008 |
| Mhe. Dkt. Mary M.Nagu (CCM) Hanang | Viwanda, Biashara na Masoko | 2008-2010 |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Dkt. Cyril A. Chami (Moshi Vijijini) | Viwanda na Biashara | 2010- sasa |

**MANAIBU MAWAZIRI**

Mhe. M.R. Kundya (Singida), Mhe.K.H.Ameir (Zanzibar), Mh.C.M.Mzindakaya (Lyangalile), Mhe. E.C.Mwanansao (Nkasi), Mh. Dk.Nicas Guido Mahinda (Morogoro), Mh.Shamim Parkar Khan (Viti Maalum), Mhe.Antony M.Diallo (Mwanza-Vijijini), Mhe.Rita Louse Mlaki (Kawe), Mhe.David Mathayo David (Same-Magharibi), Mhe.Hezekiah N.Chibulunje (Chilonwa), Mhe. Dkt. Cyrl A.Chami (Moshi-Vijijini) na Mhe.Lazaro S.Nyalandu.

**MAKATIBU WAKUU**

Bw. Fulgence Kazaura, Bw. Fadhil Mrina, Bw. Gilman Rutihinda, Bw. Ndewira Kitomari, Dkt. Fulgence J. Mujuni, Bw. Fadhil Mbanga, Bw. Silvanus Adel, Prof. Mark Mwandosya, Balozi Marten Lumbanga, Bw. Vicent Mrisho, Bw. Benard Mchomvu, Prof. Joshua Dorie, Prof. Charles Mutalemwa, Bw. Ahmada R. Ngewera, Bw. Wilfred L. Nyachia, Dkt. Stargomena L. Tax na Bibi Joyce K.G. Mapunjo.

**MANAIBU KATIBU MKUU**

Bw. Godfrey Mkocha, Dkt. Florens M. Turuka na Dkt. Shabaan R. Mwinjaka.

## 5.0 Sera na sheria zilizokuwepo tangu 1961

Katika miaka 50 iliyopita Tanzania imekuwa na Sera, Sheria na kanuni za uchumi na biashara zenye kubadilika ili kuendana na mahitaji ya nyakati husika. Mabadiliko haya yamegawanyika katika hatua tatu, ambazo ni: nyakati baada ya uhuru, nyakati za azimio la Arusha na nyakati baada ya Azimio la Arusha.

Mara baada ya nchi yetu kupata uhuru iliamua kufuatia mfumo wa siasa ya ujamaa na kujitegemea na ilipofika mwaka 1967 lilitangazwa Azimio la Arusha mbapo njia kuu zote za uchumi zilikuwa zinamilikiwa na kusimamiwa na dola ukiwemo uzalishaji viwanda na Biashara. Mashirika mbalimbali yaliundwa ili kusimamia shughuli za uzalishaji viwandani na uendeshaji biashara. Mwanzoni mwa miaka ya 1990 mfumo wa uchumi duniani ulianza kubadilika. Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ulitekelezwa ili kuendana na dhana mpya ya soko huria. Sambamba na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na uwekezaji, kiwango cha ukuaji wa uchumi kimeongezeka ambapo mchango wa ukuaji wa pato la taifa (GDP) uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 4 kwa mwaka 1986-1994 hadi kufikia asilimia 7.9 mwaka 2010. Aidha, kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa mbali mbali zikiwemo vifaa vya ujenzi na bidhaa za plastiki, nguo na vinywaji (viwanda vipya) ambapo mwanzoni

zilikuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Kutokana na mafanikio hayo, mchango wa bidhaa za viwandani katika mauzo nje na ajira umekuwa ukiongezeka.

Lengo la ubinafsishaji lilikuwa kupunguza mzigo mkubwa kwa serikali, kuiwezesha serikali kupata mapato kutokana na kuyauza mashirika hayo, kuwapa fursa Watanzania kuwekeza kwenye Mashirika hayo, kuongeza ufanisi, tija, na ubora wa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwa kuyaongezea mitaji, teknologia pamoja na menejimenti nzuri.

## 5.1 Sera za Maendeleo ya Viwanda

Wakati wa Uhuru mwaka 1961, Sekta ya viwanda Tanzania ilikuwa changa sana kutokana na uwepo wa Viwanda vichache. Wakati huo sekta ya viwanda ilikuwa ikichangia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa (GDP) na kuajiri asilimia 9 ya ajira zote. Kipaumbele kilikuwa kuendeleza sekta ya kilimo kutokana na hivyo kuifanya nchi ya kuzalisha malighafi kwa ajili ya nchi za Magharibi. Viwanda vichache vilivyokuwepo vilijikita katika usindikaji wa mazao ya kilimo na *light industries* bila kujali upatikanaji wa malighafi zilizokuwa zinapatikana nchini.

Juhudi za Mwanzo za kuweka mkakati wa kuendeleza viwanda ilikuwa katika mpango wa kwanza wa miaka mitano mwaka 1964. Mpango huu uliotoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo, ulilenga katika kuanzisha viwanda kwa kuvutia wawekezaji wa ndani vitakavyozalisha bidhaaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi *(Import Substitution)*.

Kufuatia uzinduzi wa Azimio la Arusha mwaka 1967, Serikali ilibadili mkakati wa maendeleo ya viwanda uliokuwa unalenga sera ya Ujamaa na kujitegemea. Azimio la Arusha lilijikita katika misingi miwili ambayo mkakati wa kuendeleza viwanda ulitakiwa kujikita katika misingi hiyo. Msingi wa kwanza ulikuwa kuhakikisha kuwa mkakati haulengi katika uwekezaji kwa sekta binafsi na msingi wa pili ulilenga katika kuitaifisha viwanda na mashirika yote yaliyokuwa yanamilikiwa na sekta binafsi. Mkakati wa maendeleo ya viwanda ulilenga uzalishaji ambazo zilikuwa zinaagizwa kutoka nje (import *substitution*), *intermediate and capital goods,* na viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo ( *agro-processing*) kwa ajili ya kuuza nje. Wakati huo huo msisitizo uliwekwa juu ya uendelezaji wa viwanda vinatumia nguvu kazi (*labor- intensive industries*) , viwanda vidogo na umiiliki wa viwanda pale ambapo ilonekana itasaidia kiuchumi.

Hata hivyo, maendeleo katika marekebisho ya viwanda yalikuwa na kasi ndogo sana. Mwaka 1974, serikali ilizindua mpango wa tatu wa miaka mitano uliolenga kuongeza kasi mabadiliko ya kimuundo kwenye mwelekeo wa kujitegemea. Juhudi za kuendeleza sekta ya viwanda (industrialization) ililenga usindikaji wa mazao ya kilimo na kuzalisha bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi ( import-substitution), "viwanda msingi", kukuza uwezo wa

Tanzania "kujitegemea" katika uzalishaji wa viwanda pamoja na kutimiza mahitaji ya msing ya maisha ya binadamu kwa ajili ya watanzania. "Kujitegemea" katika mazingira ya sekta y viwanda ilikuwa ikitafsiriwa kuwa uhuru wa kiuchumi.

*""Kujitegemea" katika mazingira ya sekta ya viwanda ilikuwa ikitafsiriwa kuwa uhuru wa kiuchumi"*

Tanzania iliweka kipaumbele katika *kuzalisha Basic and intemeduiate goods industries* Viwanda vya bidhaa hizo vilionekana si tu kama msingi wa mfumo wa viwanda wa nchi bal pia mhimili wa uchumi.

Sera ya *Basic Industry Strategy (BIS)*, ambayo ilipitishwa ikiwa mfumo wa msingi kwa ajil ya marekebisho ya sera ya Ujamaa Tanzania, kipaumbele kwa maendeleo ya viwanda n kuzalisha bidhaa za msingi kama chuma. Saruji na *chemicals* na sambamba na kuzalish bidhaa zitakazokidhi mahitaji muhimu ya binadamu kama chakula, malazi, afya, elimu usafiri n.k

Kuwepo kwa sera za kuongoza maendeleo ya sekta ya viwanda (*Basic Industry Strateg 1975-1995, Sustainable Industrial Development Policy –SIDP 1996-2020)* kumesaidia kulet mafanikio ya uzalishaji na ufanisi katika sekta ya Viwanda tangu wakati wa uhuru. Wizar inaendelea na utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996 – 2020) kw kutekeleza programu mbali mbali ikiwa ni pamoja na awamu ya pili ya Mpango wa Maendele ya Viwanda. Mpango huu unalenga katika kuhamasisha, kuwezesha na kuelekeza wawekezaj binafsi katika kujenga viwanda vya usindikaji wa mazao na bidhaa za kilimo ili kuongez thamani, kuongeza nafasi za ajira na kupunguza uharibifu wa mazao baada ya mavunc Moja ya mafanikio katika sekta ni pamoja na kuvumbuliwa bidhaa mpya ambazo zimesaidi kuimarisha maisha ya Watanzania, kuongezeka uwezo wa uzalishaji kwa kubadilisha n kuboresha teknolojia na uendeshaji. Wakati wa uhuru uzalishaji ulikuwa ukifanywa katik hatua ya awali zaidi (*primary processing*) tofauti na sasa ambapo uzalishaji wa bidha (*manufacturing)* umekuwa ukiongezeka sana.

## 5.2 Sera za Biashara

Mfumo wa biashara uliokuwepo baada ya uhuru ulikuwa wa soko huru na kwa kiasi kikubw uliakisi mahusiano ya wakati wa ukoloni. Sekta binafsi ilichukua nafasi muhimu ya uendeshaj na ukuzaji uchumi. Biashara ya nje na mahusiano yake yalitegemea ongezeko la uzalishaji w mazao ya kilimo na malighafi ambayo kwa kiasi kikubwa yaliuzwa nje pasipo kusindikwa Aidha, biashara ya ndani ilishabihiana na kuwepo kwa sekta kubwa ya wazalishaji amba shughuli zao za kiuchumi zilikuwa za kujikimu tu, na hivyo Sera na Sheria nyingi za wakat huo ziliweka mkazo katika uzalishaji na uuzaji wa mazao ghafi nje na wakati huo huo kuviz

hughuli za biashara ya mazao ya chakula. Hali hii iliendelea hadi mwaka 1972 ambapo Sera a Kudhibiti Biashara" ilikuwa moja ya nguzo za kutekeleza Azimio la Arusha.

era ya Kudhibiti Biashara kwa kiasi kikubwa ililenga katika kuweka shughuli zote za iashara na utoaji huduma, katika ngazi zote, ukijumuisha biashara ya jumla na rejareja, atika uendeshaji na usimamizi wa Serikali. Kufuatia hali hii na kadri ushiriki wa Serikali livyoongezeka vivyo hivyo matumizi ya nyenzo za kiutawala yaligeuka kuwa taratibu za awaida za uendeshaji biashara nchini. Nyenzo za kiutawala zilitumika kuelekeza uwekezaji, pangaji wa bei, kudhibiti uingizaji bidhaa, ugawaji na matumizi ya vibali kwa lengo la udhibiti mzunguko wa biashara na huduma katika soko la ndani. Nyenzo za kiutawala ilidhihirisha udhaifu wake pale ziliposhindwa kuhimili vishindo vilivyotokana na kupanda ei ya mafuta katika soko la dunia na kuvunjika kwa Jumuia ya Afrika Mashariki.

Iatimaye, kufikia mwanzo wa miaka ya 1980 udhaifu na athari za kudhibiti biashara zilizua ıatatizo yafuatayo:

- Kukosekana kwa ufanisi katika uwekezaji na kwa jumla kushindwa kuhamasisha uwekezaji kulikosabishwa na matumizi ya nyenzo za kiutawala katika kusimamia Sera za fedha, riba na viwango vya ubadilishji fedha
- Kuwepo kwa mfumo wa malipo usio na ufanisi wa kutosha kutokana na kutokuwepo kwa ushindani katika sekta ya fedha na kuporomoka kwa mfumo wa mikopo ya kibiashara;
- Kuvia kwa sekta binafsi na kudorora kwa vitega uchumi kutoka nje kufuatia hatua za utaifishaji mali za wawekezaji wageni na wananchi; na
- Kuvurugika kwa mfumo wa vyama vya ushirika, kutokana na kuvigeuza kuwa Mashirika ya Umma na Mamlaka za Mazao, yaliyotawaliwa na ukiritimba na utegemezi kwa ruzuku ya Serikali.

:wa ujumla hali hii ilisababisha kuibuka na kukua kwa mifumo mbadala ya masoko ya fedha a bidhaa, kiasi kwamba sehemu kubwa ya biashara nchini ilifanyika katika mfumo usio ısmi na hivyo kuathiri vibaya urari wa malipo na kuongeza pengo katika bajeti ya Serikali. :ufikia miaka ya katikati ya 1980, ilikuwa dhahiri kuwa Sera ya udhibiti wa biashara ilikuwa ıeshindwa na hivyo ilibidi yawepo mabadiliko.

## .3 Ulegezaji wa Masharti ya Biashara na Urekebishaji wa Biashara ya Ndani

Iatua za awali na zisizo rasmi katika kurekebisha sera ya biashara ya ndani zilianza mwaka

1984. Hatua hizo zilihusu ulegezaji wa taratibu za uingizaji bidhaa na usimamizi wa fedha za kigeni kwa kuwaruhusu wauzaji bidhaa nje ya nchi kubaki na kiasi fulani cha fedha za kigeni na kuzitumia kuagiza bidhaa toka nje. Hatua rasmi za kurekebisha Sera zilileta Programu ya Kurekebisha Uchumi ya mwaka 1986 na zilijumuisha kuondoa mfumo wa kupanga bei, kuondoa vikwazo dhidi ya uagizaji bidhaa kupitia mfumo wa leseni za uagizaji zisizo na pingamizi *(open general License)*. Programu hii ilianzisha hatua mbalimbali zilizolenga kuanzisha hatua kwa hatua mfumo wa uchumi wa soko unaozingatia ushindani. Baadhi ya hatua za Sera ambazo zimeanza kutekelezwa tangu wakati huo ni pamoja na:

- Utangamano wa kiuchumi kwa kutekeleza Sera endelevu za fedha na za bajeti, kama vile mfumo wa ushindani wa kiwango cha ubadilidhaji, na riba za mabenki na urekebishaji wa mfumo wa vyombo vya fedha;
- Kulegeza masharti ya biashara ya mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na kurejesha mfumo huru wa vyama vya ushirika;
- Kurekebisha mfumo wa uendeshaji na kubinafsisha mashirika ya umma katika sekta za uzalishaji, huduma na biashara;
- Kurekebisha muundo na mfumo wa uendeshaji wa Sekta za huduma, hususan, afya na elimu kwa madhumuni ya kuinua viwango vya utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wananchi wengi; na
- Urekebishaji wa muundo na mfumo wa utumishi wa umma kwa nia ya kutoa huduma bora zaidi zinazohitajika na sekta binafsi za kuweka mazingira yanayofaa kwa undeshaji biashara, ikiwa ni pamoja na kurekebisha mfumo wa Sheria na taratibu za kibiashara.

Kufikia mwaka 1996, hatua zilizotajwa hapo juu hazikufanikisha lengo la kugeuza hali ya kudumaa kwa maendeleo ya biashara nchini. Wakati huohuo, ilibainika pia kwamba hatua ya kufungua milango ya biashara pekee haitoshi katika kufufua uchumi wa nchi. Kutokufikiwa kwa malengo kulitokana na kutokuwepo kwa utaratibu unaoendeleza hatua hizo ikiwa ni pamoja na kubadili maudhui na tafsiri ya Sera ya Biashara, kutoka ile ya ndani inayolindwa na sheria na taratibu za Serikali kuelekeza zaidi katika kuhimiza ushindani wa kibiashara unaojijenga katika mfumo wa soko. Aidha, kuanzishwa kwa Shirikisho la Biashara la Dunia (WTO) na kuzidi kuimarika kwa mfumo wa utandawazi ni mambo yanayoongezea msisitizo wa umuhimu wa Tanzania kujenga uchumi unaoweza kuhimili ushindani unaojitokeza katika soko la ndani, na wakati huohuo kushiriki kikamilifu katika Jumuia za kiuchumi na katika

mfumo mpya wa biashara duniani.

## 6.0 Mabadiliko na matukio makuu kiuchumi, kiteknolojia na mafanikio yaliyopatikana hadi sasa

Mara baada ya nchi yetu kupata uhuru iliamua kufuata mfumo wa siasa ya ujamaa na kujitegema na ilipofika mwaka 1967 lilitangazwa Azimio la Arusha ambapo njia kuu zote za uchumi zilianza kumilikiwa na kusimamiwa na dola ikiwa ni pamoja na uzalishaji katika viwanda na shughuli za Biashara. Mashirika mbalimbali yaliundwa ili kusimamia shughuli za uzalishaji viwandani na uendeshaji biashara. Mwanzoni mwa miaka ya 1990 mfumo wa uchumi duniani ulianza kubadilika. Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ulitekelezwa ili kuendana na dhana mpya ya soko huria.

Sekta ya Viwanda na Biashara ni moja wapo ya sekta muhimu katika kufanikisha malengo ya ukuaji wa uchumi wa nchi na kuondoa umaskini. Sekta hii ina jukumu kuu la kuleta mabadiliko ya uchumi wa Taifa kutoka nchi maskini kufikia kiwango cha uchumi wa kati wa viwanda unaoongozwa na kilimo cha kisasa cha kibiashara chenye tija kama inavyofafanuliwa katika Dira ya maendeleo ya Taifa (*Vision 2025).*

### 6.1 Sekta ya Viwanda


Sekta ya viwanda ina jukumu kuu la kuleta mabadiliko ya uchumi wa Taifa kutoka nchi maskini kufikia kiwango cha uchumi wa kati wa viwanda unaoongozwa na kilimo cha kisasa cha kibiashara chenye tija kama inavyofafanuliwa katika Dira ya maendeleo ya Taifa *(Vision 2025).* Utekelezaji wa jukumu hilo utaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za viwandani kukidhi mahitaji ya wananchi na kuwepo kwa uchumi endelevu utakaowezesha upatikanaji wa maisha bora kwa kila mtanzania. Aidha, katika programu za MKUKUTA sekta ya viwanda imefanikiwa kuongeza kipato, kutoa ajira, kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

#### 6.1.2 Mafanikio ya Sekta ya Viwanda

Kuwepo kwa sera za kuongoza sekta ya viwanda *(Basic Industry Strategy 1975-1995, Sustainable Industrial Development Policy –SIDP 1996-2020)* kumesaidia uzalishaji na ufanisi katika sekta ya Viwanda kuongezeka tangu wakati wa uhuru. Moja ya mafanikio katika sekta ni pamoja na kuvumbuliwa bidhaa mpya ambazo zimesaidia kuimarisha maisha

ya Watanzania kuongezeka uwezo wa uzalishaji kwa kubadilisha na kuboresha teknolojia na uendeshaji. Wakati wa uhuru uzalishaji ulikuwa ukifanywa katika hatua ya awali zaidi (*primary processing*) tofauti na sasa ambapo uzalishaji wa bidhaa (*manufacturing*) umekuwa ukiongezeka sana.

**Ukuaji wa Sekta ya Viwanda 1970 – 2008**




Aidha, kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa mbali mbali zikiwemo vifaa vya ujenzi na bidhaa za plastiki, nguo na vinywaji ( viwanda vipya) ambapo mwanzoni zilikuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Kutokana na mafanikio hayo, mchango wa bidhaa za viwandani katika mauzo nje na ajira umekuwa ukiongezeka ( **Ona kielelezo juu**).

### 6.1.2.1 Mafanikio ya jumla

Katika kutekeleza wa mikakati tajwa, sekta ya viwanda imepata mafanikio makubwa. Mafanikio hayo ni pamoja ukuaji wa Sekta ya Viwanda na Mchango wake katika Pato la Taifa ambapo kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa viwandani ambalo limechangia ukuaji wa Sekta ya viwanda kufikia asilimia 9.9 mwaka 2008, kutoka asilimia 8.5 mwaka 2006 katika mwaka 2009 mchango huo ulikuwa asilimia 8.0. Aidha, mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa nao uliongezeka kutoka asilimia 8.9 mwaka 2005 na kufikia asilimia 9.4 mwaka 2008 na mwaka 2009 ulikuwa asilimia 8.6. Kupungua kidogo kwa ukuaji na mchango wa sekta ya viwanda mwaka 2009 kulitokea na adhari za mdororo wa uchumi duniani.

**Uzalishaji wa bidhaa viwandani:** Uzalishaji wa bidhaa viwandani zikiwemo konyagi, mabati,

dawa za pareto, unga wa ngano, pombe ya kibuku, saruji, bia, soda, ngozi zilizosindikwa, rangi, sigara, biskuti, tambi na nguo uliongezeka kama zinavyoonyeshwa katika jedwali lililopo hapo chini.

**Jedwali Na. 1: Ongezeko la uzalishaji wa Bidhaa (zikionyeshwa baadhi)**

| BIDHAA | MWAKA 2005 | MWAKA 2009 | ONGEZEKO (%) |
|---|---|---|---|
| Konyagi (lita) | 4,489,000 | 10,201,000 | 127.2 |
| Dawa za Pareto (tani) | 24 | 266 | 1008.2 |
| Pombe ya kibuku (lita) | 11,106,000 | 16,141,000 | 45.3 |
| mabati (tani) | 29,737 | 50,664 | 70.4 |
| Saruji (tani) | 1,366,000 | 1,941,000 | 42.1 |
| Bia (lita) | 216,604,000 | 284,906,000 | 31.5 |
| Sigara (bilioni) | 4,445 | 5,831 | 31.2 |
| Nguo na Mavazi (Mita za Mraba) | 99,134 | wastani 129,408 (2006-2009) | 30.5 |

**Utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini**: Utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini umekuwa na mafanikio ambapo usindikaji wa ngozi uliongezeka kutoka futi za mraba 6,038,000 mwaka 2005 hadi futi za mraba 37,305,215 mwaka 2009 kwa kiwango cha *wet-blue*. Mauzo ya ngozi zilizosindikwa yaliongezeka ambapo thamani yake iliongezeka kutoka shilingi bilioni 1.6 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 16 mwaka 2009. Aidha, baadhi ya viwanda vimeanza kusindika ngozi hadi kiwango cha kati - *crust leather* na cha mwisho - *finished leather* kwa ajili ya kutengenezea bidhaa za ngozi hapa nchini. Vile vile, ajira katika sekta ya viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi imeongezeka kutoka 280 mwaka 2005 hadi 520 mwaka 2009.

**Ufufuaji na uendelezaji wa viwanda vilivyobinafsishwa, uanzishwaji wa Viwanda vipya, uanzishwaji na uendelezaji wa Viwanda katika maeneo ya EPZ :** Ufufuaji na uendelezaji wa viwanda vilivyobinafsishwa, uanzishwaji wa Viwanda vipya, uanzishwaji na uendelezaji wa Viwanda katika maeneo ya EPZ na sekta ya Viwanda Vidogo kwa kiasi kikubwa vimechangia ongezeko la ajira katika sekta ya viwanda. Kwa mfano, katika maeneo

TUMETHUBUTU, TUMEWEZA, TUNAZIDI KUSONGA MBELE

ya EPZ ajira imeongezeka kutoka 3,100 mwaka 2005 hadi 9,300 mwaka 2009. Kwa ujumla, idadi ya wafanyakazi walioajiriwa katika viwanda vikubwa na vya kati walikuwa 89,316 kwa mwaka 2005 na kuongezeka hadi wafanyakazi 92,927 mwaka 2009. Katika ajira hizo, viwanda vinavyoongoza ni: viwanda vya kusindika vyakula - ajira 45,287, ufumaji na ushonaji – ajira 10,480; na Tumbaku na Sigara – ajira 7,131.

Vile vile, katika kipindi cha 2005 hadi 2009, ajira mpya 92, 547 zilipatikana kutokana na miradi iliyowezeshwa na SIDO. Hata hivyo ipo miradi mingine mingi iliyoanzishwa kutokana na mikopo na jitihada za taasisi nyingine zinazohudumia wajasiriamali wadogo. Aidha, katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa za viwandani zilizouzwa nje ziliongezeka kutoka Dola ya Marekani 156.1 milioni mwaka 2005 hadi Dola ya Marekani 497.6 milioni mwaka 2009 sawa na ongezeko la asilimia 218.

**Zoezi la ukusanyaji wa takwimu za Viwanda (Industrial Suvery):** Zoezi la ukusanyaji wa takwimu za msingi katika sekta ya viwanda kwa mwaka 2009 umekamilika na ripoti mbili kuandaliwa (i) *statitical Report na Analytical Repot.* Taarifa ilizomo katika ripoti hizi ni muhimu kwa matumizi ya wadau mbali mbali kwani zinatoa takwimu sahihi kuhusu maendeleo na changamoto za sekta ya viwanda pamoja na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa.

**Uendelezaji wa miradi mipya:** Wizara kupitia NDC imeendelea kutafuta wawekezaji wa kuwekeza na kuendeleza miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga. Kwa sasa mchakato wa kumpata mwekezaji mahiri uko katika hatua za mwisho ambapo waraka wa BLM umewasilishwa ili kupata maamuzi kuhusu mwekezaji aliyepatikana. Aidha, miradi mipya chini ya EPZ na SEZ imewezesha kupatikana kwa wawekezaji 41 wa kuanzisha viwanda mbalimbali *(EPZ pomotors)* na 36 wa kujenga miundombinu ya EPZ *(EPZ developers)*.

### 6.1.2.2 Mafanikio yaliyotokana na kukua kwa teknolojia na ubunifu


Uboreshaji katika teknojia umekuwa katika Nyanja zifuatazo:

a) Kubadili teknolojia kutoka matumizi ya mikono *(manual)* mpaka mashine zinazotumia teknolojia za kisasa *(computerized)*.
b) Mabadiliko ya teknolojia yalisababisha kuongezeka kwa bidhaa zinazotokana na malighafi ya aina fulani na kupungua kwa mabaki katika uzalishaji ( *zero-waste strategy*)
c) Kuzinduliwa kwa teknolojia za kuzalisha umeme kwa kutumia mabaki ya mimea ( mfano TANWAT, Sisal waste to biogas- ambao ni mtambo mkubwa zaidi duniani unaozalisha umeme kwa kutumia mabaki ya mkonge)
d) Viwanda vilianza kuzalisha nishati kutokana na mabaki ya shughuli za uzalishaji ( mfano



*...idhaa za nguo zitokanazo na pamba zinazozalishwa nchini*

**Sekta y... vya Ngozi:** Mabadiliko makubwa yametokea katika sekta ya ngozi na bidhaa ... adiliko haya ni kutokana na kuongezeka kwa bidhaa mpya zinazotokana na malig... ozi. Sekta ya viwanda vya ngozi imepiga hatua kubwa katika kutengeneza ngozi ... ngozi ambapo wakati wa uhuru ni viwanda vichache tu vilikuwa vikisindika ngozi k... o cha wet blue wakati sasa kuna viwanda nane vya kusindika ngozi kati ya hiyo ... ndivyo vinavyofanyakazi. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inateke... kati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya ngozi.



*Ngozi ambayo haijaongezwa thamani*



na mat... teknolojia za kisasa na uongezekaji wa mitaji katika viwanda hivi. Wakati wa



*Kiwanda cha kuongeza thamani ngozi katika kiwango cha wet blue.*



*Viatu vya ngozi vilivyotengenezwa na wajasiriamali nchini.*


Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa uboreshaji na ukusanyaji wa ngozi umefanyika pamoja na kuongeza uwezo wa kusindika ngozi na utengenezaji wa bidhaa za ngozi hapa nchini. Ili kutekeleza mkakati huo wizara inaandaa vijiji vya viwanda katika kanda 4 na baadae maeneo mengine yataongezwa.

Pamoja na usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi zitokanazo ngozi za mbuzi, ng'ombe na kondoo, kumekuwepo na bidhaa za ngozi za wanyama pori, samaki, nyoka na mamba.



*Mh. Dr. Cryil Chami, Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara, akiangalia kiatu kilichotengenezwa na Moja ya kiwanda cha Ngozi nchini.*

**Viwanda vya Bidhaa za Ujenzi:** Hii ni sekta ambayo uwekezaji umekua ukiongezeka mwaka hadi mwaka tokea wakati wa uhuru. Viwanda vipya vilivyoanzishwa kutokana na sekta binafsi ni pamoja na viwanda vya saruji na vigae, viwanda vya kuyeyusha vyuma, viwanda vya mabati, viwanda vya misumari na *"fancing wires"*, viwanda vya kutengeneza nyaya za shaba kwa ajili ya umeme.



*Moja ya Kiwanda cha Saruji nchini*

**Sekta ya Viwanda vya Plastiki na Magodoro:** Sekta ya Viwanda vya plastiki inajumuisha viwanda vya kutengeneza mabomba ya maji na shughuli zingine, viwanda vya kutengeneza bidhaa za nyumbani, viwanda vya kutengeneza mifuko ya plastiki na vifungashio vya plastiki viwanda hivi vimeweza kuhimili ushindani kutokana na ubora wa bidhaa zake. Ushidani mkubwa katika bidhaa za plastiki hasa kwa bidhaa/vyombo vya matumizi ya nyumbani ulikuwa kwa bidhaa kutoka Kenya. Lakini kwa sasa viwanda vyetu vimeboresha teknolojia na hivi sasa vinatoa bidhaa bora zaidi kuliko bidhaa za Kenya. Aidha uzalishaji wa magodoro katika miaka ya 1960 ulikuwa unatumia nyuzi za katani na sufi tofauti na sasa ambapo magodoro yanayozalishwa ni ya "foam" kwa kutumia kemikali.

**Sekta ya Madawa ya Binadamu:** Miaka 30 baada ya uhuru kulikuwa na viwanda vichache vya kutengeza madawa. Tokea mwaka 2000 uzalishaji wa madawa nchini umekuwa ukiongezeka kutokana na uanzishwaji wa bidhaa mpya za madawa. . Viwanda hivi pia vimeweza kupata sifa ya uzalishaji bora *(Good Manufacturing Practices – GMP*) ambayo ni sifa muhimu katika viwanda vinapozalisha madawa ya Binadamu. Uzalishaji katika viwanda hivi unakidhi asilimia sitini (60%) ya madawa yanayotumiwa hapa nchini.

**Sekta ya Viwanda vya Vyakula:** Sekta hii imeonyesha maendeleo makubwa ukilinganisha

na hapo awali i hapakuwa na viwanda vya kukoboa na kusaga nafaka hali iliyosababisha walaji kutumia vinu vya kienyeji kutengeneza unga au kukoboa mpunga. Aidha viwanda vya kukamua na kutengeneza mafuta ya kula ni eneo lililoonyesha mafanikio makubwa na kuenea katika maeneo kadhaa ya vijijini katika mikoa mbali mbali kama vile mkoa wa Singida, Kigoma na Dodoma. Viwanda vingine vilivyoonesha mafanikio makubwa ni katika bidhaa kama mikate,juisi, biskuti, chumvi, sukari na minofu ya samaki.

**Sekta ya Vinywaji:** Viwanda vya vinyaji baridi na moto vimepata mafanikio makubwa baada ya sekta binafsi kukabidhiwa shughuli za uzalishaji. Aidha, kumekuwa na bidhaa mpya kama vile maji ya chupa, aina mpya za bia, mvinyo, vinywaji vikali (Konyagi) na soda. Maji ya kunywa ya chupa ni bidhaa mpya ambayo ina manufaa makubwa kwa afya za wananchi.

Ice Cream



Fruit juice



Bottled water




### 6.1. 2. 4 Mafanikio katika Utafiti na Maendeleo

Taasisi za utafiti, teknolojia na ubunifu za sekta ya viwanda ziliweza kubuni na kuendeleza teknojia mbalimbali.

Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (**TEMDO**) mashine na mitambo zaidi ya sitini ya kukamua na kuchuja mafuta ya alizeti na mbegu nyingine za mafuta,mashine za kupukuchua na kupepeta mahindi zenye uwezo wa kilogramu 2500 kwa saa, mashine za kutetefya na kusindika matunda, mtambo wa kukamua na kusindika mafuta yatokanayo na michikichi, mashine za kusindika maziwa, mashine na vifaa vya kusindika asali na bidhaa za asali,mtambo wa kutengeneza vyakula vya mifugo mashine ya kuweka dawa kwenye mbegu (Seed dressing equipment), mtambo wa kuchoma taka za hospitali na taka ngumu (Hospital/ Solid Waste Incinerator) na teknolojia ya kutengeneza mkaa na kuni unaotokana na mabaki

ya mimea.



Katika kipindi cha takriban miaka 30 cha kuwepo kwake, Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijini (CAMARTEC) imebuni na kuunda teknolojia mbalimbali ambazo zimewanufaisha watumiaji moja kwa moja.Teknolojia hizo ni pamoja na pampu ya maji ya kina kifupi na ile ya umwagiliaji mashambani, mkokoteni wa kusambaza mbolea mashambani, mkokoteni wa kuvutwa na wanyama kazi kwa ajili ya usafirishaji, majembe ya kukokotwa na wanyama kazi, vipandio vya mbegu mbalimbali, mashine za kutengeneza tofali na vigae vya kuezekea kwa ajili ya nyumba za gharama nafuu, matenki ya maji ya ujazo mbalimbali ya kuvunia maji ya mvua, mashine za kukatakata majani kwa malisho ya wanyama, mashine za kupura mazao kama vile mpunga au mtama, mashine za kusindika mazao na zile za kukamua mafuta, teknolojia za kutumia nishati ya mionzi ya jua kuchemshia maji na kwa kupikia, teknolojia ya biogesi, teknolojia ya kutumia nishati ya nguvu za upepo kusukuma pampu za maji na teknolojia za majiko sanifu na banifu ya kutumia mkaa na kuni.






*Mhe. Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania akikagua Trekta lililotengenezwa na Kituo cha Utafiti wa Zana za Kilimo CARMATEC wakati wa Maonesho ya Nanenane, Dodoma..*

Aidha pamoja na mafanikio hayo ya jumla, hivi karibuni Kituo kimepata mafanikio mahsusi na makubwa katika uundaji wa teknolojia za zana za kilimo na zile za nishati ikiwemo uundaji wa trekta dogo lenye matumizi mbalimbali. Uenezi wa mitambo ya kati ya biogesi ya

kuzalisha umeme wa KW 16 unafanyiwa uchunguzi katika kijiji cha Msoga (Chalinze, Mkoa wa Pwani).



*Faida mbalimbali zitokanazo na Bio-gas katika michoro*

Mitambo mitatu yenye jumla ya meta za ukubwa wa ($m^3$)450 tayari imekwisha kujengwa. Aidha,mtambo miwili ya biogesi inayotumia mfumo wa mitambo ya "Biolatrine" yenye ukubwa wa meta za ujazo 40 kila mmoja na kueneza teknolojia ya biogesi tangu mwaka 1983 ambapo zaidi ya mitambo midogo 5000 imejengwa maeneo mbalimbali nchini na nje ya nchi.




*Faida mbalimbali zitokanazo na Bio-gas katika michoro (kabla na baada ya kutumia Bio-gas)*

Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) lenye jukumu la kufanya utafiti unaolenga kuongeza thamani ya malighafi inayopatikana nchini kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya ndani na kuuza nje ya nchi limefanya tafiti mbalimbali zikiwemo kuzalisha *"Sodium Alganate"* kutokana na kaolin, kuzalisha *"Caustic soda"* kutokana na magadi soda, uzalishwaji wa *furfural* na *furane resines* kutoka katika mabaki ya *pentosan*, utengenezaji wa "*essential oil*" kutokana na majani kama michungwa , michaichai, utunzaji wa bidhaa za mbao, utafiti wa sumu ya *Ochratoxin A* katika kahawa, utafiti wa kuboresha uyoga, utafiti wa kuboresha unga wa muhogo na matumizi bora ya nishati. Aidha, Shirika limeweza kutengeneza mashine mbalimbali zikiwemo Mashine ya kuparaza muhogo (*cassava grating machine*), mashine ya kukamua mafuta ya mawese kutoka katika mchikichi (*palm oil*

*processing machine),* mashine za urejeshaji taka (*paper and plastic recycling plant)* ambapo wajasiriamali zaidi ya 150 walifundishwa na wengine kuanzisha viwanda vyao.

Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO) liliaanzishwa mwaka 1973 kwa ajili ya kupanga, kuratibu na kutoa huduma mbalimbali kwa viwanda vidogo nchini. Tangu kuanzishwa kwake imewezesha kuanzishwa na kuendeleza viwanda vidogo kwa kutoa huduma na msukumo katika maeneo ya utafutaji na usambazaji wa teknolojia, utoaji wa mafunzo mbalimbali, kusaidia uhimili wa ushindani wa soko na mikopo.



*Moja ya mashine za kukoboa mahindi zinazotengenezwa na SIDO*

Shirika limeweza kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo **108,297** na kutengeneza ajira za moja kwa moja **560,406.** Viwanda hivi vinajumuisha vile vilivyoanzishwa kwenye mitaa 18 ya SIDO na vipo mijini na vijijini. Aidha limeweza kuendesha mafunzo kwa wajasiriamali **173,827** katika mikoa yote ya Tanzania bara na kutengeneza ajira **67,279** . Mafunzo haya yalilenga ufundi chuma, useremala, useketaji, usindikaji na uhifadhi wa vyakula matunda na mbogamboga, ufinyanzi, bidhaa za mianzi, utengenezaji wa chaki, sabuni, mishumaa, usindikaji ngozi na utekenezaji bidhaa za ngozi, utengenezaji wa mizinga ya nyuki ya kisasa na uchakataji wa asali.

### 6.1.2. 5 Ujenzi wa miundombinu ya viwanda na uwekezaji

Wizara ya viwanda, Biashara na Masoko iliona umuhimu wa kuweka mikakati thabiti ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda. Hii ilikuwa ni muhimu kutokana na mabadiliko ya kisisasa na kiuchumi katika nchi yetu ambapo serikali ililazimika kujitoa katika shughuli za kibiashara na kuiachia sekta binafsi. Mabadiliko hayo yalisababisha uanzishwaji wa Shirika la Maendeleo la Taif na Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji (EPZA).



*Eneo la Benjamin Mkapa EPZA*

Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji imeweza kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo ya EPZ na SEZ; kujenga miundombinu ya Maeneo Maalum ya viwanda; kutoa lesseni za EPZ na SEZ na pia kutoa huduma mbalimbali za uwekezaji kwa ufanisi na uharaka. Maeneo ya EPZA yanayofanya kazi mpaka sasa ni pamoja na Millenium Busines Park iliyopo Dar es Salaam, Hifadhi Industrial Park EPZ iliyopo Dar es Salaam, Benjamin William Mkapa SEZ iliyopo Dar es Salaam, Vector Health EPZ- Kisongo, iliyopo Arusha, Kamal Industrial Park EPZ, iliyopo Zinga, Bagamoyo, Pwani na Global Industrial Park iliyopo Mkuranga, Pwani. Maeneo haya yamewekewa miundombinu yote ya misingi ikiwamo mabarabara, uzio, nishati za umeme na gas, na mifumo ya maji safi na maji taka. Wawekezaji huweza kukodi ardhi ama majengo ya viwanda na kuanza kufanya biashara kwa uharaka bila bugudha na katika mazingira mazuri yenye huduma zote na miundombinu ya kimataifa.

Hadi sasa Makampuni 74 yamekwisha kupewa leseni za EPZ ambapo leseni 35 zimetolewa kwa Ujenzi wa Majengo ya Viwanda na leseni 39 zimetolewa kwa uanzishwaji wa viwanda. Hadi sasa kiasi cha uwekezaji wa EPZ umefikia jumla ya USD 650 milioni, imeweza kutoa ajira za kudumu 13,000, mauzo ya nje ya nchi yamefikia jumla ya USD 350 milioni, asilimia 35 ya uwekezaji chini ya program zote mbili (EPZ/SEZ) ipo kwenye viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini (Agro-processing).

Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) limefanya utafiti na kubaini kuwa kuna jumla ya kiasi cha tani milioni 454.1 za makaa ya Mchuchuma. Kiasi kilichohakikiwa ni tani milioni 125.3. Kufuatana na uhakiki uliofanyika hivi karibuni na Mtaalam Mwelekezi, mgodi wa Mchuchma unaweza kuzalisha tani million tatu kwa mwaka (3.0MT/mwaka) za makaa ya mawe ambayo yatazalisha umeme wa nguvu ya Megawati mia sita (600MW) na kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

NDC ikishirikiana na uongozi wa Wilaya ya Ludewa na Mthamini wa Serikali imewaelimsha wananchi wa maeneo ya mradi kuweza kupokea zoezi la uthamanishaji wa mali na taratibu za fidia, ikiwa ni pamoja na kupata takwimu muhimu kwa ajili ya ufanikishaji wa zoezi hilo. Sambamba na elimu, mipaka ya maeneo ya mradi imebainishwa na lengo ni kutambua wananchi walio ndani ya eneo la mradi. Zoezi la kutathimini mali zilizomo ndani ya maeneo ya miradi na ulipaji fidia litafanyika wakati wa utekelezaji.

Shirika pia linaendeleza mradi wa makaa ya mawe ya Ngaka katika Mkoa wa Ruvuma kwa ubia na mwekezaji binafsi wa kampuni ya *Pacific Corporation East Africa (PCEA)* ambayo ni kampuni tanzu ya *Atomic Resources Ltd ya Australia*. NDC na PCEA wameunda kampuni ya *Tancoal Energy Limited* ambayo inaendeleza mradi huu.

Tafiti zilizofanyika hivi karibuni zimebaini kuwa kuna jumla ya kiasi cha tani millioni 179 za mkaa na kiasi kilichohakikiwa ni tani milioni 118.4. Kampuni ina mpango wa kuzalisha jumla ya tani milioni mbili kwa mwaka za makaa ambayo yatazalisha umeme na kuingiza kwenye gridi ya taifa wa nguvu ya Megawati mia nne (400MW). Utafiti wa makaa ya mawe katika sehemu zingine za Ngaka unaendelea pamoja na tafiti za awali za kuanzisha kituo cha kuzalisha umeme na athari za mradi katika mazingira na jamii katika mradi huo wa kuchimba makaa ya mawe na kuzalisha umeme.

Uwekezaji unalenga kukamilika na kuanza mgodi wa makaa (tani milioni mbili kwa mwaka) na kituo cha umeme (megawati 400) ifikapo 2013. Hata hivyo changamoto kubwa itakuwa katika ujenzi wa mtandao wa msongo wa umeme *(Transmission Line)* wa kilovoti 400.

Shirika linategemea kuingiza jumla ya umeme wa nguvu za megawati elfu moja (1,000MW)

katika gridi ya Taifa kutoka Mchuchuma na Ngaka kutokana na makaa ya mawe.

Mradi wa mchuchuma na liganga kwa sasa umekwishawapata wawekezaji baada ya mchakato wa zabuni uliofanyika na kupata makampuni kumi ambayo yalionyesha nia ya kuja kuwekeza katika miradi hiyo na tayari kandarasi hiyo imepewa kampuni ya SICHUAN HONGDA

Mradi huu utakuwa na faida kubwa katika uimarishaji wa uzalishaji viwandani kutokana na upatikanaji wa umeme wa ukahika pamoja na kuimarika kwa viwanda vya msingi kwa maendeleo ya uchumi kutokana na upatikanaji wa chuma.

Aidha pia utasaidia kwa serikali kupata mapato na kodi katika mlolongo wa uongezaji wa thamani za madini ya chuma na makaa ya mawe pamoja na nchi kufaidika na kupatikana kwa teknolojia na fursa za ajira kwa wananchi.

Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) pia limetenga eneo la Maganga Matitu ambayo ni sehemu ya Liganga wilayani Ludewa lenye ukubwa wa kilomita za mraba 14.33 (kwa ajili ya chuma) na eneo la Katewaka lenye ukubwa wa kilomita za mraba 28.4 (kwa ajili ya makaa ya mawe) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Shirika vile vile lilitangaza zabuni kwa lengo la kuwapata wawekezaji wa ndani wenye uwezo wa kuzalisha chuma ghafi *(sponge iron)*.

*Kampuni ya MM Steel Resources Public Limited (MMSRPL)* ya Dar es Salaam ilishinda zabuni hiyo ili iungane na NDC kuendeleza Mpango huo. NDC na MMSRPL wameunda kampuni ya *Maganga Matitu Resource Development Ltd* kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji wa chuma ghafi. Aidha, utekelezaji wa miradi yenye tafiti na changanuo za kitaalamu zilizokamilika uliendelea na hatua iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

- Ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Mbamba Bay umebakiza vipande vya barabara kati ya Tunduru – Mangaka na Mbinga-Mbamba Bay ambavyo bado havijapata ufadhili.
- Zoezi la kuunganisha/kujumuisha utekelezaji wa mradi wa matumizi ya rasilimali ya makaa ya mawe umeanza
- Utafiti wa uanzishaji na uchimbaji wa raslimali ya Gesi na Petroli unaendelea
- Ujenzi wa Daraja la Umoja "Unity Bridge" baina ya Tanzania na Msumbiji umekamilika kwa gharama ya shs. 28 milioni na ufunguzi ulifanyika tarehe 12 Mei 2010. Ujenzi ulianza tangu mwaka 2006 ukigharimiwa na Serikali za Tanzania na Msumbiji.
- Vile vile, ujenzi wa barabara ya Tunduma – Sumbawanga unaendelea baada ya

kupata fedha kutoka MCC.

Shirika limeendelea na juhudi za kutafutiwa wawekezaji kwa ajili ya miradi mingineyo na hatua mbali mbali za utekelezaji zilifiiwa. Uuanzishwaji wa mashamba ya majaribio ya "Woodchips" ambayo yanafanywa na OJI Paper ya Japan ulianza sambamba na tathimini ya athari ya mradi kimazingira.

**Mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma:** Mradi huu unahusu mgodi, uzalishaji wa umeme na matumizi ya viwandani. Mwekezaji tayari amepatikana kuanzisha mgodi **tani milioni 3 kwa mwaka**, kituo cha kuzalisha umeme **megawati 600** na makazi kwa jumla ya **Dola Za Kimarekani bilioni 1.10.** Mradi unataraji kukamilika mwaka 2014/2015. Msongo wa umeme wa 400 kV utahitajika kuunganisha kwenye gridi ya taifa kadri ya Kilomita 300 hadi Iringa.

**Mradi wa Chuma cha Liganga**: Mradi huu unahusu Uchunguzi, Mgodi **tani milioni 2.5 kwa mwaka**, Ufasishaji wa miamba ya chuma, uchenjuaji na uzalishaji wa aina mbali mbali za chuma kibiashara **tani milioni moja kwa mwaka** na kutumia jumla ya **Dola Za Kimarekani billioni 1.80.**

**Mradi wa Makaa ya Mawe ya Ngaka:** Mradi huu unahusu uchimbaji wa makaa ya mawe kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi ya viwandani. Mwekezaji tayari amepatikana kwa ajili ya kuanzisha mgodi **tani milioni 2- 5 kwa mwaka**, kituo cha kuzalisha umeme **megawati 60 X 2 Ngaka na 1,000 Kyela** na makazi.

**Mradi wa Kasi Mpya wa Kuzalisha Chuma Ghafi Maganga Matitu**: Mradi huu unahusu Uchunguzi, Mgodi, Ufasishaji wa miamba ya chuma, uchenjuaji na uzalishaji wa aina mbali mbali za chuma kibiashara na kutumia jumla ya **Dola Za Kimarekani millioni 150.** Mradi utakuwa katika sehemu tatu:

- Mgodi wa kuchimba chuma tani 812,000 kwa mwaka.
- Ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha chuma ghafi tani 330,000 kwa mwaka
- Mgodi wa kuchimba makaa ya mawe Katewaka tani 340,000 kwa mwaka.
- Kuzalisha umeme kutokana na hewa ya joto toka DRI metawatti 45
- Ujenzi wa Makazi na miundombinu inayohusiana na mradi.

Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zake inaratibu maboresho katika maeneo ya kuanzisha, kuendesha na kufunga biashara.

**Kuanzisha na kufunga biashara:**

Katika kuanzisha na kufunga Biashara, maeneo ambayo mpaka sasa yanaendelea kufanyiwa maboresho ni pamoja na Kubadilisha mfumo wa sasa wa usajili na uandikishaji kutoka kwenye mfumo wa makabrasha(manual) kwenda kwenye mfumo wa kielektroniki na kufanya marekebisho ya Sheria. Baadhi ya maboresho yaliyotokea pamoja na mafanikio yake ni pamoja na:

(a) Kuanzishwa kwa Nambari ya Utambulisho wa mlipakodi 'TIN' badala ya cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi (BLTC). TIN hutambulisha na humwezesha mlipakodi kuanzisha biashara nyingine mahali popote nchini bila kupitia ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania katika eneo analofungua tawi la biashara. BLTC ilikuwa inatolewa kwa kila eneo(Wilaya) ambalo mfanyabiashara anafungua biashara na inaendelezwa kila mwaka.

(b) Kutungwa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara Namba 14 ya mwaka 2007 ambayo itaifuta sheria ya zamani ya leseni za biashara ya mwaka 1972 ili kuondoa ukiritimba na vikwazo katika utoaji wa leseni za biashara.

(c) Kutungwa kwa Sheria ya usajili wa Makampuni Namba 12 ya mwaka 2002 *(The Companies' Act. 2002) ambayo* imeifuta Sheria ya zamani ya Makampuni *(Companies Ordinance Cap 212).* Sheria hii imerahisisha masharti *(Insolvency Rules)* ya kuandikisha makampuni, kuendesha na kufunga kampuni.

(d) Kuanzishwa kwa mahakama maalumu '*High Court Commercial Court Division*'. Mahakama hii hushughulikia kesi na migogoro ya kibiashara kwa haraka zaidi,

(e) Kuweka mfumo wa kuhifadhi majina ya biashara yaliyosajiliwa.
Mfumo huu umewezesha kupungua kwa muda wa kuhakiki jina la biashara na kampunni (*Name search and Name clearance*) hadi siku moja.

(f) Matumizi ya TEKNOHAMA katika usajili wa majina ya biashara na uandikishwaji wa makampuni. Hili limewezesha upatikanaji kiurahisi wa taarifa na utoaji wa

huduma za usajili. Mfano BRELA imeweka katika tovuti yake *(www.brela-tz.org)* taarifa zote zihusuzo huduma inazozitoa ikiwa ni pamoja na fomu za maombi ya usajili wa makampuni, majina ya biashara, alama za biashara na huduma, hataza, fomu za maombi ya leseni za viwanda, Katiba ya kampuni *(Memorandum and Articles of Association)* ya mfano. Katiba hii imewezesha wanaosajili kampuni wanaweza kuutumia mfano huu wa katiba badala ya kuingia gharama za kuandaa nyaraka hizi.

(g) Kuongezeka kwa makampuni yaliyoandikishwa na majina ya Biashara yaliyosajiliwa

(h) Kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TANTRADE Act)* Namba 4 ya mwaka 2009 badala ya Sheria ya Halmashauri ya Biashara ya Nje ya mwaka 1975. Sheria hii inasimamia na kuratibu biashara ya ndani na nje. Sheria hii imepunguza idadi ya taasisi ambazo zingehitajika kusimamia biashara ya ndani na ya nje.

(i) Kutungwa kwa Sera za Masoko ya Mazao ya Kilimo (2008); Sera ya Taifa ya Biashara (2003); Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara ndogo (2003) na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996-2020). Sera hizi zimewezesha sekta binafsi kuwa sekta kiongozi katika maendeleo ya uchumi.

(j) Kusajiliwa kwa kampuni inayoshughulikia mfumo wa utambuzi wa bidhaa *(Bar Codes)(GS 1(TZ) National Limited. Hii* itawezesha bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kutambulika kitaifa na kimataifa katika uuzaji wake. Wazalishaji wengi hapa nchini wanaweza kuuza bidhaa hizo katika soko la kimataifa. Kabla ya hapo bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zilikuwa zinatumia nembo ya *Bar Codes* katika nchi ya Kenya na Afrika Kusini. Faida za kuwa na utambuzi wa bidhaa hapa nchini ni:-

- Uboreshaji wa udhibiti wa mfumo wa usambazaji,
- Ubora na usalama wa bidhaa,
- Kulinda thamani ya jina la bidhaa,
- Rahisi kujumuisha taarifa nyingi za kuwezesha kutambua bidhaa, nchi ilikozalishwa bidhaa husika, mfumo wa uzalishaji, ubora na usalama wa bidhaa na ufuatiliaji wa bidhaa(traceability)

za Serikali, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ununuzi wa bidhaa za ndani kwa kupitia kauli mbiu ya 'NUNUA BIDHAA ZA TANZANIA JENGA TANZANIA' thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje (f.o.b) ilipungua kwa asilimia 10.9 na kufikia Dola 5,775.7 mwaka 2009. Upungufu huo ulichangiwa na kupungua kwa uingizaji wa bidhaa za kati ambazo ni mafuta, mbolea na malighafi za viwandani.

### 6.2.5 Vituo vya pamoja vya Mpakani


Vituo vya Pamoja vya Mpakani ni vituo vinavyojumuisha Taasisi za usimamizi wa shughuli za mipakani za nchi husika kwa nia ya kutekeleza majukumu yao kwa pamoja. Taasisi hizo za kiserkali ni pamoja na Uhamiaji, Mamlaka za Mapato na Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Kwa kufanya kazi kwa pamoja inawezesha watu, magari na bidhaa kukaguliwa mara moja wakati wa kuingia au kutoka katika mpaka wa nchi..

Mfumo huu utaleta ufanisi wa kufanya kazi mipakani tofauti na hali ilivyo sasa ambapo watu, magari na bidhaa hulazimika kukaguliwa katika sehemu zote mbili za mipaka. Sehemu nyingi duniani utaratibu huu umekuwa unatumika, kwa mfano Jumuia ya Ulaya, mpaka wa Marekani na Kanada, Asia na Amerika kusini. Mfumo huu pia unatumika Afrika katika mpaka wa nchi ya Zambia na Zimbabwe, katika mpaka wa nchi ya Togo na Burkina Faso na pia katika mpaka wa Kenya na Uganda katika kituo cha Malaba.

Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kutambua umuhimu wa Vituo vya Pamoja vya Mpakani kama nyenzo muhimu ya kuongeza ufanisi wa kufanya biashara mipakani na pia kuongeza ufanisi wa biashara kati nchi yetu na majirani zake imeanzisha mazungumzo na nchi jirani ya Zambia ili kutiliana saini mkataba utakaowezesha kuanzishwa kwa Kituo cha Pamoja cha Mpakani cha Tunduma/Nakonde.



**OSBP CHIRUNDU; MPAKANI MWA ZAMBIA NA ZIMBABWE**




MASHINE YA KUKAGUA MIZIGO

### 6:2:5:1 Faida za Vituo vya Pamoja vya Mpakani

Vituo vya Pamoja vya Mpakani vina faida nyingi kwa wafanyabiashara, uchumi wa nchi, na watumiaji wa huduma za mpakani. Faida hizi ni pamoja na :-

- Kuongezeka kwa ufanisi wa kufanya biashara kwa kuwezesha upitaji wa watu, magari na bidhaa mipakani kwa urahisi na uharaka zaidi hivyo kupunguza muda unaotumiwa mipakani na pia kuwaondolea gharama wafanyabiashara wanaotumia huduma za hapa nchini kwetu.
- Kuvutia watumiaji wa bandari yetu na hivyo kuhamasisha ongezeko kubwa la biashara za huduma na usafirishaji.
- Kuchangia katika ongezeko la ukubwa wa kibiashara na pia pato la wananchi kwa ujumla.
- Kuhamasisha kwa upatikanaji wa ajira kwa wananchi wetu kutokana na ukweli kwamba kutakuwa na mahitaji makubwa ya huduma na watoa huduma hizo ni wananchi wetu.
- Kuondoa vishawishi vya kutumia njia za panya, kuondoa urasimu na kuongeza makusanyo ya mapato.




**URAHISI WA ABIRIA KWA KUFANYIWA UKAGUZI MARA MOJA**

**6:2:5:2 Matarajio ya wadau wa Vituo vya Pamoja vya mpakani**

Vituo vya Pamoja vya Mpakani vikianza kazi ni matarajio ya wadau kuona kuwa huduma za mpakani zinaboreshwa hii ikiwa ni pamoja na :-

- Vituo hivi kuwa wazi masaa ishirini na nne ili kuondokana na tatizo la tofauti za masaa kati ya nchi na nchi lakini pia kutoa huduma muda wote wakati inapohitajika.
- Kuwa na usalama wa watu, magari na bidhaa zaidi ili kuwawezesha wadau kutumia huduma hizi muda wowote.
- Kuwa na mifumo sawa ya **TEKNOHAMA** kwa ajili ya kurahisisha shughuli za mipakani
- Kuwa na vitendea kazi vya kisasa mipakani kama vile scanner. Kwa vitendea kazi hivi kazi zitachuwa muda mfupi zaidi.
- Kuwepo kwa maeneo ya kutosha na makubwa ya maegesho ya magari. Maeneo haya yawe na taratibu nzuri za kisasa na pia yawe na usalama wa magari yenyewe, bidhaa na madereva.
- Kuwepo kwa maghala ya kuhifadhia bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na maghala maalumu kwa ajili ya bidhaa zinazoharibika kwa urahisi.(Warehouses

and cool room facilities)


- Kuwepo kwa huduma za kifedha yaani matawi ya benki lakini pia ATM ili kuzuia ubebaji wa pesa nyingi suala ambalo ni hatari.
- Kuwa na maafisa wa huduma za mpakani wenye uweledi wa kutosha kwenye taaluma ya huduma wanayotoa.

### 6:2:5:3 Maeneo kwa ajili ya Vituo vya Pamoja vya Mipakani

Vituo vya pamoja mipakani vilivyo katika mpango wakuendelezwa haraka ili kuhakikisha kuwa Tanzania inatumia kikamilifu fursa za kibiashara zinazotokana na nchi tunazopakana nazo na vilevile kuanzishwa kwa soko la pamoja kwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kutumia fursa za kibiashara zilizopo COMESA na SADC. Vituo vya mipakani vinavyopendekezwa kuendelezwa ni pamoja na:-

(i) Mtukula katika Wilaya ya Missenyi (mpaka wa Tanzania na Uganda).

(i) Kabanga katika Wilaya ya Ngara (mpaka wa Tanzania na Burundi).
(ii) Rusumo katika Wilaya ya Ngara (Mpaka wa Tanzania na Rwanda).
(iii) Sirari katika Wilaya ya Tarime (mpaka wa Tanzania na Kenya).
(iv) Namanga-Wilaya ya Longida (Mpaka wa Tanzania na Kenya).
(v) Holili- Wilaya ya Rombo (Mpaka wa Tanzania na Kenya).
(vi) Holoholo –Wilaya ya Mkinga (Mpaka wa Tanzania na Kenya).
(vii) Umoja Bridge- Mtwara (Mpaka wa Tanzania na Msumbiji).



Ujenzi au uendelezaji vituo vya ukaguzi Mipakani ni hatua muhimu katika kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na nchi jirani. Kwa kuwa Tanzania ipo kwenye mchakato wa kuingia katika soko la pamoja kwa nchi za Afrika Mashariki, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali ina jukumu la kujenga na kuendeleza vituo vya ukaguzi mipakani ili kupunguza gharama za kufanya biashara na kufanikisha biashara na nchi jirani.

### 6.2. 6.1 Ushindani huru na wa haki

Uimarishaji wa fursa sawa katika soko hurahisisha wafanyabiashara kuingia au kutoka katika soko hilo bila vipingamizi na hivyo huchochea maendeleo ya ubunifu wa teknolojia mpya, bidhaa na huduma bora zaidi za aina mbalimbali na hukuza fursa za uchaguzi kwa mlaji. Haya yote kwa ujumla wake yanawezesha kukua kwa sekta ya biashara ndogo, za kati na kubwa na kuchochea ushindani wa biashara katika kukidhi mahitaji na matarajio ya mlaji kuhusiana na huduma na bidhaa hizo.

Kwa upande wa uchumi, ushindani huleta ufanisi wa utendaji wa kiuchumi na hukidhi maslahi ya mlaji ambaye ndiye kitovu cha kukua kwa biashara na uchumi.

Tume ya Ushindani imeendesha misako katika maingilio ya bidhaa kwenye bandari, Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam, maduka na maghala katika jiji la Dar es Salaam, mipaka ya Sirari na Holololo na katika baadhi ya mikoa ikiwemo Mwanza, Tanga, Singida, Ruvuma na Mbeya kwa nia ya kukagua uwepo wa bidhaa bandia. Juhudi hizo zimeiwezesha kukamata na kuteketeza bidhaa bandia zenye thamani ya Sh. Bilioni 3.2 kati ya mwezi Mei, 2007 na Desemba, 2010. Aidha Tume imetoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu shughuli zake na athari zinazosababishwa na bidhaa bandia. Elimu hiyo imetolewa kwa Asasi za Kiraia katika Mikoa ya Mwanza (2007), Arusha (2008), Dodoma (2008) na Mtwara (2008).

### 6.2.6.2 Kuongezeka kwa ubora wa bidhaa

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) tangu kuanzishwa kwake limepata mafanikio mengi katika utekelezaji wake wa majukumu yake ya uwekaji viwango vya ubora wa bidhaa na usimamiaji wa utekelezaji wa viwango hivyo.

Shirika hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2010 limetayarisha viwango vya kitaifa 1400 katika sekta mbalimbali ambazo ni pamoja na kilimo na chakula, nguo, kemikali, uhandisi, na mazingira na viwango vya Afrika Mashariki vinavyofikia **1,222** vimekamilishwa katika nyanja za uhandisi, vyakula, nguo na kemikali.. Shirika pia liliendelea kusimamia utekelezaji wa viwango vya taifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora (*certification schemes)*. Hadi kufikia mwezi Desemba 2010 Shirika lilikuwa limetoa jumla ya leseni 1,138 za ubora wa bidhaa mbalimbali katika viwanda 762 vya ndani ya nchi. Aidha jumla ya viwanda

vidogovidogo 162 vya ndani ya nchi vimepatiwa leseni baada ya kuthibitishwa kuwa vinazalisha kulingana na Viwango vya Kitaifa ambavyo huwaruhusu kutumia alama ya "tbs" ya ubora wa bidhaa.

Shirika limeendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Desemba 2010 Shirika limetoa jumla ya leseni 11,312 za ubora wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje. Aidha Shirika limeanzisha vituo vya mipakani mwa nchi ambavyo ni Tanga (Bandarini na Horohoro – Tanga/Mombasa), Holili (Moshi/Taveta) na Sirari (Mara/ Kisumu), Sirari (Mara/Kisumu) na Namanga.

Shirika limetoa mafunzo kwa wafanyakazi viwandani 7,310 wa ngazi mbalimbali, wakiwemo wafanyakazi wa ngazi ya chini, wasimamizi, mameneja, na watendaji wakuu kuhusu umuhimu wa viwango na udhibiti wa ubora wa bidhaa. Vile vile kuanzia mwaka 2007 Shirika kupitia ufadhili wa UNIDO linaendelea kutoa huduma za maabara ya ugezi inayotembea (mobile calibration van) katika sehemu mbali mbali hapa nchini.

### 6.2.6.3 Kuboresha biashara ya ndani.

Idara imeendelea kuratibu kwa mafanikio Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Dar es Salaam International Trade Fair) mwezi Julai kila mwaka, Madhumuni ya maonesho haya ni kukuza biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani kwa kuzitangaza bidhaa za viwandani, sanaa za mikono, madini na utalii unaopatikana nchini kuvutia Wawekezaji.

### 6.2.7 Utoaji wa elimu na mafunzo ya biashara (CBE, SIDO, TANTRADE)

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kilianza na idara moja ya uongozi wa biashara yenye michepuo mitatu ya Masoko, Uhasibu na Ugavi. Kutokana na ongezeko la mahitaji ya elimu ya biashara, Chuo kilianzisha idara zingine za mafunzo ya Mizani na Vipimo, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Hadi sasa Mafunzo yanayotolewa katika ngazi za astashahada, stashahada, shahada na stashahada za juu.

Chuo kilidahili wanachuo 28 mwaka 1965 katika fani ya Uongozi wa Biashara, hata hivyo idadi ya wanachuo waliodahiliwa iliongezeka hadi kufikia 10,704 mwaka 2010.

Chuo kimefungua Kampasi nyingine mbili ambazo ni Kampasi ya Dodoma iliyofunguliwa mwaka 1983 kwa kuanza na udahili wa wanachuo 240 na Kampasi ya Mwanza iliyofunguliwa mwaka 2007. Hadi mwaka 2011 Kampasi ya Dodoma ina wanachuo 3080 wengi wao wakiwa ni kutoka mkoa wa Dodoma na mikoa jirani ya kanda ya kati na Kampasi ya Mwanza ina wanachuo 1746 kutoka wanachuo 288 waliodahiliwa Mwaka 2007 wengi wa wanachuo hutoka kanda ya ziwa na mikoa jirani.

## 6.3 Sekta ya Masoko

### 6.3.1 Kuboreshwa kwa masoko

Wizara kupitia Idara ya Uhamasishaji wa Biashara na Masoko, BRELA, SIDO na Wakala wa Vipimo, imefanikiwa kusajili Biashara, Majina ya makampuni na Vikundi vya Biashara ili kuwa na Biashara zilizo rasmi mipakani na kunufaika na soko la EAC na SADC. Aidha, Wizara imeshatoa elimu na kusajili vikundi vya Biashara zaidi ya 50 katika mipaka ya Namanga (Arusha), Holoholo (Kilimanjaro), Horiri (Tanga), Sirari na Shirati (Mara), Mtukula (Kagera), Mtambaswala (Mtwara), Manyovu (Kigoma), Kipiri, Kirando, Kasesya, na Kasanga(Rukwa) na Tunduma na Kasumulo (Mbeya).

Aidha, Wizara kupitia Idara ya Uhamasishaji Biashara na Masoko imefanikiwa kujenga Masoko yanayokidhi viwango vya Kimataifa na hivyo kuwawezesha wakulima kuuza Mazao yao yakiwa katika ubora. Mfano wa masoko hayo ni Kibaigwa iliyoko Dodoma, Kinole na Mgeta yaliyoko Morogoro. Pia kwa sasa Wizara inajenga masoko yaliyo katika hadhi ya Kimataifa katika maeneo ya Segera – Tanga na Makambako mkoani Iringa.



*Masoko ya kisasa yenye miundombinu, Soko la Kibaigwa, Dodoma*



*Masoko ya zamani hayana miundombinu, Soko la Ngara na Sirari*

### 6.3.2 Kuboresha utoaji wa lesseni

Idara imeweza kuendelea kutoa huduma ya utoaji wa Leseni za Biashara zenye sura ya Kimataifa na kitaifa zaidi ya 11,000 kwa kipindi cha mpaka Februari, 2011

Wafanyabiashara wameweza kurasimisha biashra zao kwa urahisi zaidi kwa vile sasa hivi Leseni hizo za Biashara zinatolewa bila ya gharama yeyote.

### 6.3.3 Utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara BARA

Kuanzishwa kwa mfumo wa Usajili wa Shughuli za Biashara chini ya Sheria ya BARA kumesaidia kwa kiwango kikubwa kutoa usumbufu waliokuwa wanaupata wafanyabiashara pale wanapohitaji kusajili shughuli zao za kibiashara. Wizara imeshatoa Mafunzo ya kutumia Mfumo wa Usajili wa Shughuli za Biashara chini ya Sheria ya BARA kwa Maafisa Biashara wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, na utekelezaji umeshanza katika wilaya 24, Pia mipango inaendelea kuweza kuzifikia wilaya zote 109 zilizobaki.

### 6.3.4 Kukamilika Uandaaji wa Sera ya Leseni za udhibiti, Sera ya Masoko na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Masoko.


Kulikuwa na tatizo la muda mrefu katika sekta ya kilimo ambalo lilisababishwa na kutokuwepo kwa muongozo/ sheria inayolinda sekta hiyo na mkulima kwa ujumla, kwa hivyo kukamilika kwa Sera ya Masoko ya (2008) na Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo (2011), kumesaidia kuyapatia ufumbuzi matatizo sugu ya kunyonywa kwa wakulima kwa kupangiwa bei, kukusekana kwa taasisi zinazokopesha wakulima, na sasaMazao na bidhaa za kilimo zinauzwa kwa utaratibu wenye manufaa kwa wakulima,

Aidha kukamilika kwa Sera ya Leseni ya Udhibiti kumesaidia kupunguza mlolongo wa taratibu ambazo zilikuwa chini ya sheria na mamalaka mbalimbali na sasa Sera imejenga mazingira bora ya kufanya biashara wa wawekezaji wa ndani na nje.


Kwa upande wa Sera ya Masoko na mkakati wake umesaidia wakulima kupata bei nzuri za mazao yao.

### 6.3.5.0 Kuboresha mfumo wa masoko ( mfumo wa stakabadhi ghalani)

Mabadiliko ya mfumo wa masoko tangu wakati wa uhuru uliathiri mfumo wa masoko kwa bidhaa za mazao ya kilimo hususa mazao ya biashara kama korosho , kahawa na pamba. Baada ya shughuliza kibiashara kuwekwa mikononi mwa sekta binafsi wakulima waliyumbishwa sana juu ya bei na kupelekea kuuza, kwa mfano korosho, kwa watu wa kati au walanguzi kwa bei ya chini sana. Hali hii iliwanemeesha watu wa kati. Kutokana na mazingira haya katika soko serikali ililazimika kutafuta utaratibu mbadala wa kuboresha uuzaji mazao kwa lengo kumkomboa mkulima.



*Moja kati ya maghala mapya 28 yalijengwa na kusajiliwa kwa ajili ya kuendesha Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani kwa ajili ya Korosho, Mtwara*




*Moja kati ya maghala mapya yaliyosajiliwa kwa ajili ya kuendesha Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani kwa ajili ya Alizeti, Singida*

Kuanzishwa kwa mfumo wa skakabadhi za mazao ghalani mwaka 2007 umeweza kutengeneza mazingira ya ushindani katika ununuzi wa mazao hali iliyosababisha wakulima kuwa na uhakika wa bei za mazao wanayozalisha. Mfano bei ya Korosho kwa kilo imeongezeka kutoka shilingi 340 msimu wa mwaka 2000/01 hadi shilingi 890 katika msimu wa mwaka 2008/09, kahawa iliyokobolewa kutoka shilingi 1,020 msimu wa mwaka 2004/05 mpaka shilingi 2,340 katika msimu wa mwaka 2008/09.

### 6.3.5.1 Uhakika wa bei ya bidhaa


Kutokana na mfumo kutengeneza mazingira ya ushindani katika ununuzi wa mazao, wakulima wamekuwa na uhakika na bei za mazao wanayozalisha. Aidha, mtiririko wa bei kama jedwali hapa chini linavyoonyesha zimekuwa zinaimarika kwa kiwango kizuri mwaka hadi mwaka. Halmashauri katika maeneo husika pia zimenufaika kupitia kodi kutokana na ongezeko la bei.

| MWAKA | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Korosho (Tshs/Kg) | 340 | 370 | 360 | 550 | 750 | 600 | 610 | 675 | 980 |
| Mpunga (Tshs/Kg) | 230 | 250 | 270 | 280 | 300 | 464 | 550 | 475 | 500 |
| Pamba (Tshs/Kg) | 56.9 | 99 | 110.25 | 109.8 | 179.2 | 143 | 291.6 | 346.5 | 297.6 |
| Kahawa (Tshs/Kg) | - | - | - | - | 1,020 | 1,440 | 1,800 | 2,160 | 2,340 |




### 6.3.5.2 Mkulima kuunganishwa na asasi za fedha

Kupitia mfumo huu mkulima amepata uwezo wa kuomba na kupata mikopo kutoka asasi za fedha kama mabenki ya biashara kwa kutumia mazao aliyoyahifadhi ghalani kama dhamana ya mkopo.



Aidha, taasisi za fedha zinamsaidia mkulima kuwa na taarifa za kutosha kuhusu mweka mali, mwendesha ghala na bidhaa zitakazohifadhiwa. Asasi za faedha zinatakiwa kuhakikisha zinatoa mkopo unaozingatia bei na gharama zote atakazotumia mweka mali.

Ikumbukwe kuwa nje ya utaratibu huu ni vigumu sana kwa mkulima wa kawaida kijijini kuweza kupata mkopo toka benki kwani wakulima wengi hawana dhamana zinazotambulika kisheria.

**6.3.5.3 Mikopo iliyotolewa kwenye vikundi na Asasi za fedha 2009/10**

| MAZAO | KIASI (Tshs Bilioni) | ENEO | BENKI |
|---|---|---|---|
| Kahawa | 27 | Kilimanjaro, Mbeya | CRDB |
| | 1.6 | Ruvuma na Kilimanjaro | KCC |
| Korosho | 25 | Lindi, Mtwara na Pwani | NMB |
| | 14 | Lindi na Mtwara | CRDB |
| Mpunga | 10 | Kilimanjaro, Mbeya na Morogoro | CRDB |
| | 0.7 | Kilimanjaro | KCB |
| Mahindi | 3 | Kilimanjaro, Morogoro na Manyara | CRDB |

Mikopo iliyotolewa kwa vikundi na wanachama wa vyama vya msingi wanaohifadhi mazao kwenye maghala chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

**6.3.6.0 Kuboresha mfumo wa ununuzi wa mazao.**


Wakala wa Mizani naVipimo inajukumu la kumlinda mlaji kwa kuhakikisha anapata bidhaa kupitia matumizi ya vipimo sahihi katika ununuzi na uuzaji. Wakala mpaka imesogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua ofisi katika mikoa yote ya Tanzania bara na kwa mkoa wa Dar es Salaam kila wilaya ina ofisi ya Vipimo. Aidha Wakala imeweza kuongeza idadi ya vipimo vinavyokaguliwa kutoka vipimo **200,000** mwaka 2002/20003 hadi vipimo**740,000** katika mwaka 2009/2010 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 270 ikiwa wastani wa ongezeko la asilimia 45 kila mwaka. Wakala pia imeongeza maeneo mapya ya kazi ambayo ni pamoja na ukaguzi wa malori ya mchanga, matanki ya makubwa yakuhifadhia mafuta ya juu na chini ya ardhi, ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa, ukaguzi wa mita za maji. Wakala pia imeongeza usimamizi wa sheria kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara hatua iliyosababisha kunasa wakiukaji wa sheria 9,330 mwaka 2009/2010 kutoka wakosaji 427 mwaka 2005/2006.

### 6.3.7.0 Utoaji wa taarifa na tafiti za masoko

Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Idara ya Uhamasishaji, Biashara na Masoko inasimamia na kuratibu mifumo ya taarifa za masoko ambayo imekuwepo kwa takribani miaka 20 sasa. Idara imekuwa, katika kipindi chote hicho, ikitoa vitendea kazi na mafunzo ya kujenga uwezo kwa wakusanya taarifa sanjari na kuboresha mifumo hiyo pale inapohitajika.Mifumo hiyo ni;

- **Mfumo wa Taarifa za Masoko ya Mazao ya Kilimo (FAO Agri Market System – FAM)**. Mfumo huo una taarifa zinazohusisha jumla ya masoko 93 yaliyopo katika makao makuu ya mikoa yote ya Tanzania Bara na katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya. Taarifa zinazokusanywa ni bei za jumla kwa mazao makuu ya chakula ya aina (8) yaani maharage, mahindi, ulezi, mtama, uwele, viazi mviringo na mchele na hukusanywa mara tatu (3) kwa wiki; bei za rejareja, bei za mkulima na bei za pembejeo na zana za kilimo ambazo hukusanywa mara mbili kwa mwezi. Taarifa hizi.

- Aidha, Idara inaratibu na kusimamia Mfumo wa Taarifa za Masoko ya Mifugo (Livestock Information Network and Knowledge System - LINKS) ambao unakusanya taarifa za masoko ya mifugo katika minada 58 iliyopo katika Wilaya 46. Taarifa zinazokusanywa ni Bei, Idadi, Madaraja ya ubora kwa jinsia na Gharama za usafirishaji wa Mifugo. Hii inahusu Mifugo na mazao ya Ng'ombe, Mbuzi, Kuku, Kondoo, Ngamia, Maziwa na Ngozi. Mfumo huo unatumika na kuunganishwa kwa nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Ethiopia. Taarifa hizi hutolewa kwenye Magazeti ya kila siku, Radio, Luninga na kupitia ujumbe wa simu za kiganjani, hivyo zimesaidia sana katika kufungua fursa za masoko na ku promote market transparency na pia kuwasaidia wadau katika sekta ya biashara kutumia taarifa hizi kufanya uchambuzi, na maamuzi mbalimbali ya kibiashara ndani ya sekta hiyo.




*Taarifa za bei ya masoko ya nje mikoani ikiwa katika moja ya mbao za masoko kwa ajili ya wadau*

### 6.3.8.0 Fursa za masoko (maonyesho ya bidhaa ndani na nje, TANTRADE, SIDO, Vituo vya Biashara – Dubai, London)

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TAN TRADE) imekuwa ikiratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonyesho mbalimbali ya Biashara ya Kimataifa ya nje ya Nchi kwa mfano, Rwanda, Namibia, Kenya, China, Afrika ya Kusini Msumbiji, Malawi, Botswana, Zambia n.k

TANTRADE imeratibu misafara ya Kibiashara inayoingia nchini na inayotoka nje, kwa lengo la kukuza biashara kwa mfano misafara ya wafanyabiashara wa Tanzania nchini Marekani, India, China n.k.

Mamlaka imeratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonyesho makubwa ya EXPO ambapo wajasiriamali wengi wameshiriki, kama vile Expo Aichi, Expo Shanghai, Expo Zaragoza n.k.

Mamlaka imeratibu Maonyesho ya bidhaa za kitanzania (Solo Exhibition), Maonyesho haya yalihusisha bidhaa za kitanzania yalifanyika katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Msumbiji ambapo wajasiriamali na wafanyabiashara wa Tanzania walipata fursa ya kuuza bidhaa zao.

Kwa takribani miaka arobaini sasa kila mwaka Mamlaka imekuwa ikiratibu Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambayo yamekuwa ya mafanikio makubwa na kukutanisha Wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi. Aidha Tantrade imeanzisha Maonyesho ya Kisekta ambayo yanatoa fursa zaidi kwa wajasiriamali wa sekta moja kubadilishana uzoefu, kupeana taarifa za masoko na kuuza bidhaa zao.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ina majukumu ya kusajili Kampuni za ndani na nje ya nchi ambapo kwa kipindi cha miaka kumi jumla ya kampuni 39,407 zimesajiliwa kutoka idadi ya kampuni 2,949 zilizokuwa zimesajiliwa mwaka 1999/2000, Usajili wa majina ya Biashara tayari majina 77,100 yamesajiliwa kulinganisha na majina 3,467 kwa mwaka 1999/2000, Alama za Biashara na huduma 3,738 zimesajiliwa hadi sasa kutoka alama 800 kwa mwaka 1999/2000, Hataza *(Patents)* zimesajiliwa 228 kutoka alama 9 kwa mwaka 1999/2000 na Leseni za Viwanda 381 zimesajiliwa toka 76 kwa mwaka 1999/2000. Kwa kipindi cha miaka kumi sasa BRELA imerahisisha taratibu za usajili wa makampuni na Majina ya biashara hatua iliyopunguza muda wakusajili kampuni kuwa kati ya siku 3 hadi 5 na usajili wa majina ya biashara kufanyika kati ya siku 1 hadi 3. Aidha Wakala sasa unasajili alama za biashara (Patent) hapa nchini tofauti na kipindi cha nyuma ambapo usajili ulikuwa ukifanyika nchi Uingereza.

### 6.3.9.0 Uanzishaji na uimarishaji wa Haki miliki (COSOTA)

Kumekuwepo ongezeko la wasanii wanaoshugulika na masuala ya hakimiliki mfano wasanii wa muziki wameongezeka sana hususan wasanii wa muziki wa injili na bongo fleva na pia kumekuwepo na kuwepo kwa usambazaji wa muziki uliopendwa miaka ya nyuma. Kumekuwepo pia na wasanii wengi wanayojishugulisha na filamu na maigizo, sanaa za uchoraji na uchongaji, uchapaji, usanifu, upigaji picha za sinema na kazi nyingine za vielelezo vya kuona na kusikia; sanaa ya litografia namapambo; kazi za mikono au zinazotengenezwa katika viwango vya viwandani; uchoraji ramani na michoro na jiografia,topografia, usanifu wa majengo au sayansi.

Kazi hizi hulindwa punde tu zinapokuwa katika mfumo wakushikika hata kabla ya kusajili, hivyo usajili husaidia katika kusimamia na kupunguza migogoro juu ya umiliki. Kumekuwepo pia na ongezeko la makampuni yanayoshugulika na masuala ya hakimiliki mfano Makampuni mengi yameongezeka yanayojishugulisha na uzalishaji na usambazaji wa muziki, filamu na maigizo, machapisho, sanaa za uchoraji na uchongaji, usanifu, upigaji picha za sinema na kazi nyingine za vielelezo vya kuona na kusikia; sanaa ya litografia na mapambo; kazi za mikono au zinazotengenezwa katika viwango vya viwandani;uchoraji ramani na michoro na jiografia, topografia, usanifu wa majengo au sayansi. Kazi hizi hulindwa punde tu zinapokuwa katika mfumo wa kushikika hata kabla ya kusajili, hivyo usajili husaidia katika kusimamia na kupunguza migogoro juu ya umiliki.

Aidha, toka sheria ya hakimiliki imekuwepo na kupelekea COSOTA kuanza kazi mwaka 2004, imesajili wanachama 2099 na kazi 11322 ambapo ni dhahiri pia kuwa kuna wabunifu na kazi nyingi ambazo hazijasajiliwa hivyo ni dhahiri kuwa kuna tofauti kubwa sana ya jinsi ilivyokuwa kabla ya uhuru na miaka 50 baada ya uhuru. Vilevile kumekuwepo na kushughulikia masuala ya uharamia na ulipaji mirabaha na kesi mbalimbali zinazohusu hakimiliki zinaendelea katika mahakama za hapa nchini Tanzania.

## 7.0 Changamoto

### 7.1 Changamoto zilizojitokeza katika ngazi ya Wizara

Kutengewa fedha katika bajeti za kutosha kutekeleza majukumu ya sekta na kazi zilizopangwa ili kuweza kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa Taifa.

- Kuendeleza na kuiwezesha sekta binafsi ili itekeleze majukumu yake kama mhimili mkuu wa uchumi
- Kuchukua hatua za makusudi za kuwalinda wazalishaji dhidi ya biashara isiyo halali hususan kutoka nje

- Kuhakikisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji na biashara
- Kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, biashara na masoko
- Kuhakikisha uzalishaji wa mazao na bidhaa unakidhi mahitaji ya ubora unaotoa ushindani katika soko la ndani na nje
- Kuendeleza na kujenga uwezo wa wajasiriamali wa kuibua na kutumia fursa za uzalishaji, biashara na masoko.
- Kuendeleza na kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotumia malighafi za hapa nchini ili kuongeza uzalishaji, ajira na pato la Serikali
- Kujenga uwezo wa Taasisi za utafiti na huduma utakaowezesha kubuni na kuendeleza teknolojia bora na za kisasa
- Ufahamu mdogo wa matumizi ya TEKNOHAMA,
- Kukosekana kwa Nishati ya umeme ya uhakika na ya kutosheleza kuendesha mifumo,
- Uelewa mdogo wa wadau kuhusu sheria na kanuni zinazosimamia biashara,
- Miundombinu ya barabara,umeme, mawasiliano, maji, reli, bado duni,

### 7.2 Changamoto katika ngazi za Taasisi

**Sheria:** Kumekuwa na mkanganyiko wa sheria inayohusu NDC kwa kuzingatia kuwa sheria iliyoianzisha ya mwaka 1965 bado inatumika sambamba na ile ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992. Hii inatoa mkanganyiko ukizingatia kuwa Sheria hiyo inatoa fursa kwa NDC kubinafsishwa wakati wowote.

**Mtaji:** NDC inahitaji mtaji kwa ajili ya majukumu yake kwa kuwa haina chanzo chochote cha mapato cha kuaminika na kilicho katika mstari wa majukumu yake.


**Miundombinu ya Umeme:** Uwezo mdogo na miundombinu iliyochakaa ya msongo wa umeme kwa kiwango cha 220 kV badala ya 400 kV ni kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa Miradi ya umeme ya Mchuchuma na Ngaka ambayo katika kipindi cha miaka minne hadi kumi imejipanga kuongeza jumla ya MW 1,800 kwenye Gridi zaidi ya mara mbili ya kiwango cha sasa cha MW 830.

**Miundombinu ya Usafirishaji:** Uwekezaji unaohitajika katika miradi mikubwa ya Migodi ya Liganga na Mchuchuma ni Reli na Bandari ya Mtwara kwa kiwango kikubwa ambacho hakijatokea katika nchi nyingi za Kiafrika. Aidha, uwekezaji katika miradi hii utawezesha nchi kutekeleza Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda na Dira ya Maendeleo ya Taifa.

**Umuhimu wa Kumiliki Rasilimali:** Umiliki wa madini hasa yale ya viwanda (*strategic industrial minerals*) ni muhimu sana Serikali ikayatenga na kuhakikisha kuwa yanasimamiwa na taasisi zake kama NDC ili yafanyiwe tafiti za kina na kuwa kichocheo cha uchumi na kivutio kwa wawekezaji kama ilivyokwishadhihirika katika miradi ya Mchuchuma, Ngaka, Liganga na Magadi ya Ziwa Natron.

### 7.3 Matararajio ya Wizara na Taasisi katika miaka hamsini (50).

Wizara pamoja na Taasisi zilizochini yake itaendelea kubuni mikakati na mipango ya kutekeleza majukumu yake ili kuongeza mchango wa Sekta ya viwanda, biashara na masoko katika pato la taifa. Aidha Wizara kupitia taasisi zake itaendelea kuweka umuhimu katika Taasisi kama NDC katika kujenga na kuimarisha uchumi wa nchi, na hasa kuhakikisha umiliki na uendelezaji wa raslimali ili Watanzania waweze kufaidika.




MIAKA HAMSINI YA UHURU TANZANIA BARA

1961 - 2011